KONGAMANO LA MWEZI-UKUMBI WA EACROTANAL
ZANZIBARA TAREHE 22/5/1991 – 23/5/1991.

Mjadala wa mwezi ulikuwa ni sehemu ya kongamano lililotolewa anuani ya "Semina ya ."Kiislamu Zanzibar

Mada nyengine zilizojadiliwa kwenye semina hiyo ni Sala ya Ijumaa na Adhuhuri, Makaburi, Khitma na mambo anayofanyiwa maiti, Maulid na talaka tatu. Sisi tutachukua .mjadala wa mwezi tu, uliochukua nafasi zaidi

Semina ilifunguliwa na aliyekuwa rais wa Zanziabar bwana Salmin Amour Juma na yeye .ndiye aliyeifunga

Masheikh maarufu waliohudhuria semina hiyo ukiondoa watoa mada ni pamoja na marehemu Skh Ameir Tajo, Skh Ameir Tajo mdogo, Skh Nurdeen Hussein Shaadhily. .Hawa ni wachache tu niliowataja kutoka ukumbi uliojaa

Miaka imekuwa mingi tangu semina hiyo ifanyike, hali za walioshiriki zimebadilika. Wengine wamebadilika nyadhifa na wengine si hai tena. Ninao wafahamu mimi ni wachache. Hivyo katika kuwataja, nitawataja kwa utangulizi wa hadhi zao kama .ninavyowajua au walivyotambulishwa siku hiyo

Ukumbi ulipambwa na bango lenye aya ya 103 ya Surat, Al Imran(3) yenye kuhimimza .mshikamao wa Waislamu
Semina ilifunguliwa kwa usomaji wa Qura'an na kijana aliyeisoma kutoka Surat Anfal. Ikafuatiwa na sheikh aliyetoa utangulizi na autambulisho wa Semina kwa wageni kutoka kote Afrika Mashariki.

Baada ya kuzitaja mada ambazo zingezungumzwa kwa siku mbili za semina, sheikh huyo ambaye inaonesha alisimama kwa niaba ya Serikali, alitoa matumaini yake, kuwa matarajiao ni kuwa baada ya semina kumalizika pangepatikana maelewano mazuri baina ya waislamu, kwani alisema mada zile zilizochaguliwa ni zenye mitizamo tofauti na ndizo .zenye kusababisha kutokuelewana huko baina yao

Ni matarajio kuwa mwisho wa semina waislamu wangepata rai ipi ya kufuata. Akafuatia .kumkaribisha Kadhi Mkuu wa Zanzibar; marehemu Sheikh Ameir Tajo

Sheikh Ameir Tajo naye, akasimama kumkaribisha Rais wa Zanzibar, msheshimiwa .Salmini Amour Juma

Baada ya rais kusalimiana kwa utangulizi wa kiada ya Uislamu na kiitifaki ya kiserikali akasema: Tumekutana, kuzungumzia masuala makubwa yanayohusu dini yetu. Nimepata faraja kuja kwenu, kwani ni kipimo jinsi gani mumeshiba imani. Ndugu wageni, nataraji .mutashirikiana vizuri ili ipatikane manufaa iliyokusudiwa

Kumekuwa na tafsiri tofauti za aya na hadithi za Mtume (S.A.W) Jambo ambalo ni la .kutahadhari, ni kuzipa nguvu tofauti hizo mpaka zikatugawa

Mifarakano imekuwepo tangu enzi za Mtume (S.A.W) na baada ya kufa. Mimi binafsi nimeshuhudiana mifarakano mibaya kuhusu suala la sala ya Adhuhuri na Ijumaa hapa Zanzibar na hasa mashamba.Pia nimeshuhudia mifarakano mibaya zaidi kule Bukoba .iliyoleta hasara kuhusu suala hili

Tulipata fursa ya kutatua hili la Ijumaa na Adhuhuri. Tatizo la Bukoba likatoweka. .Tulirejesha hali ya amani mpaka leo

Ndugu wanavyuoni; haifai kujenga mawazo finyu juu ya hali hii na kuanza kubabaika juu ya mambo yanayotokea. Tanzania ni sehemu ya dunia.Kumeanza kutokea watu wenye kutofautiana katika kutafsiri baadhi ya mambo. Kuwepo kwa semina hii kutasaidia kuwakutanisha baadhi ya masheikh kujadiliana kwa undani juu ya tofauti hizi, kwa lengo la .kuyapatia ufumbuzi na msimamo unaohusu misingi ya dini

Kwa hakika katika dini ya Uislamu kumekuwepo mambo mengi yenye kuwaunganisha waislamu wote tangu Mtume (S.A.W), na wala hayategemewi kubadilika. Kwa mfano kuwa ulimwengu huu umeumbwa na Mola mmoja asiye na mshirika. Pia kwamba kila muumini ni kwa ajili ya kumuabudu Mwenyezi Mungu. Kadhalika maelekezo ya masahaba .yametoa ufafanuzi mzuri

Kuna maelezo ya Mtume (S.A.W), kumekuwa na milima ya ufafanuzi, lakini bado kuna tofauti katika jitihada za wanavyuoni na uvumbuzi wa kisayansi na maendeleo ya .kiteknolojia. Bado tofauti zimeendelea kuwepo

Katika kipindi hiki ambapo kuna vuguvugu la madhehebu ya dini, baadhi ya watu wameona ikiwa tofauti hizo zitaachwa kuendelea, zinaweza hata zikaathiri misingi ya dini .yenyewe

Wengine wameona kuwa, tofauti hizi zinaweza zinaweza zikaleta mzozo mkubwa unaow eza kuondoa hali ya utulivu miongoni mwa waislamu wenyewe kwa wenyewe.Wako watu wanafikiria tofauti hizi ni upungufu wa taaluma za kidini. Mawazo haya yanadhihirisha .kuwepo tofauti za mawazo na taaluma za kidini

Hivyo ni vyema kwa masheikh na maulamaa kukutana ili kuweka sawa yale yote .yanayoleta mifarakano

Miongoni mwa mambo makubwa ni suala la tofauti za kuandama kwa mwezi na jinsi ya waislamu kufuata ili kuendeleza ibada zao za funga. Pia kama ratiba inavyosema semina .itajadili khitama, dhikri, maulid, sala ya ijumaa na adhuhuri

Ni mategemeo kuwa semina hii ya siku mbili itafanya mengi makubwa katika kutetea na kupata ufumbuzi wa kitaalamu na ili kuihami dini hii ya Uislamu, na kutoa maelezo sahihi .ya kufuatwa na kila muislamu na kila muumini. Mungu ataleta kheri

Nyote mutatumia juhudi za wajibu wenu na kutumia Uislamu kwa kuelekezana usahihi wa dini hii inavyotaka. Na kamwe fikra za mtu binafsi zisizotokana na kitabu cha Mwenyezi .Mungu na suna sahihi za Mtume (S.A.W) hazitopata nafasi katika mjadala huu

Hali hii itafikiwa kwa kuweka mbele utukufu wa dini badala ya tamaa, ubinafsi au sifa .katika utukufu wa dunia

Wanavyuoni muna jukumu kubwa kuhakikisha kuwa vijana wetu wanaeleweshwa misingi .ya dini kwa mapenzi, maelewano na umoja

Visiwa vya Zanzibar vina histori kubwa kidogo. Masheikh waliotangulia walijitahidi kupanda mbegu za matumaini mema ya mapenzi katika dini na taqwa. Sote tunamkumbuka Skh Abdallah Saleh Farsiy kwa kazi kubwa aliyoifanya hapa Zanzibar ya kusomesha watu .na Afrika Mashariki yote

Hata mara moja sheikh Abdallah Saleh Farsy hakutamka maneno ya kuleta mfarakano. Na hata alipokwenda Mombasa alihimiza mshikamano na masheikh aliowakuta huko. Je .haitoshi kuutumia mfano wa Skh Abdallah Saleh Farsiy kama mfano wa karibu

Natarajia masheikh mumejitayarisha vya kutosha katika kutoa hoja ya mambo yatakaosaidia waumini kujua pa kushika na pa kuacha juu ya mambo haya yenye kuleta .utatanishi mkubwa kwa waumini

Natumai pia mjadala huu utawasaidia waumini hasa vijana kuelewa barbara misingi ya dini yao ili kutambua tofauti iliyopo kati ya imani ya Mungu na ili kulinda umoja na .umadhubuti wa taifa

Waumini wanapaswa kuepuka hila zote zinazoweza kuleta mfarakano nchini, kwa mujibu .(wa njia zilizowekwa kwenye Qur'an na Suna za Mtume (S.A.W

Jukumu la kuleta umoja ni la watu wote, na hasa waumini wa dini. Lakini ieleweke kuwa jukumu la kulinda amani ni la watu wote na hasa dola. Serikali itajitahidi kushirikiana na watu wote na hasa vyombo vya dini, isipokuwa kama hali ya utulivu itahatarishwa na mtu .mmoja au kikundi cha watu wachache

Naomba ieleweke na nadhani ndivyo inavyoeleweka, kuwa tafauti kama hizi katika masuala ya fiqh sio msingi wa kuwatenganisha waislamu. Wala isiwe sababu ya .madhehebu haya kuyatia dosari madhehebu yale

Naamini kuwa yote hayo ni jitihada za maulamaa katika kuzifahamu aya za Mwenyezi .(Mungu na hadithi za Mtume (S.A.W
Tatizo la msingi linalojitokeza katika masuala haya si kuzuia mijadala ya elimu. Mijadala .ya elimu ndio maendeleo ya elimu yenyewe

Watu lazima waulize na wajibiwe, wapatiwe ufafanuzi. Ndugu wanavyuoni nawaombeni kuwasomesha waumini mambo ambayo yatamsaidia muumini huyo kuyaelewa barabara .misingi ya imani yake na haja ya maelewano na wenzake

Ni vyema kwa mazingira yetu tuzingatie umoja wetu katika kuendeleza dini, ili taifa letu liwe na maslahi. Sitarajii semina itakuwa na pande mbili za kulia na kushoto. Mwenyezi .Mungu anasema; Enyi waumini msigombane ili umoja wenu usije ukapotea

Nawakaribisha wageni wote kutoka nje ya Zanzibar na wote wengine. Na Semina .natangaza imefunguliwa rasmi

Baada ya kumuaga rais aliyeondoka kuendelea na shughuli nyengine, wajumbe wa semina .walikwenda kupata chai n a viburudisho halafu wakarudi ukumbini kuendelea na semina

Waliporudi mwenyekiti alikuwa ni skh Ahmad Zuberi Ahmadi, ambaye aliwataka watoa .mada watakaoanza punde wasiende ndani sana katika kufahamisha ili watu wote wafaidike

Mtoa mada wa mwanzo alikuwa awe Ahmad Majid Ali lakini jalada lilionesha angezungumza Ahmad Muhammad Msalam. Wote hawa ilikuwa ni masheikh kutoka Mombasa nchini Kenya. Baada ya marekebisho skh Ahmad Msallam alichukua nafasi na .kuwasilisha hoja zake zilizowakilisha hoja za Ansaar Suna

Baada ya kumshukuru Allah (S.W) na kuwatakia rehema Mtume (S.A.W) na ahli zake na masahaba kwa ujumla, akawashukuru waandalizi wa semina ile kwa ihtimamu zao kubwa -:za kusimamia Uislamu na akaendelea kwa kusema

Mwenyezi Mungu akimdhalilishia mtu kwa jambo tukufu na mtu huyo naye ni mtukufu. Wanaolitumikia jambo hili nao ni watukufu. Mtume (S.A.W) amesema asiyewashukuru .watu na hamshukuru Mungu (S.W),palipobakia Allah (S.W) ataliongoza ili lifanikiwe

Nimevutiwa na aya kwenye bango; Wa-atassi-muu bihablilaah …. Kamba kikwetu ni ingwe.Nitalifasiri kipande kipande ili tupate madhumuni hasa ambayo yako ndani ya aya .hii

Nisingekuwa na haja ya kuifasiri sana aya hii, kwani mheshimiwa rais tayari amejaribu kwa hutba ya muongozo. Mengi tuliyosikia kutoka kwa rais. Lakini kwa vile kila mtu ana mchango kwenye jambo; na mimi ningependa nipewe nafasi na wasikilizaji ili nitoe mchango wangu.

Mwenyezi Mungu baada ya kutuzungumza nyuma, kabla kipande cha aya hii “wa atassimuu “- shikamaneni. Hii ni amri wanapewa baadhi ya watu wenye tabia fulani- A, Certain class of people.Na sote tunajua waliopewa amri hii ni waumini.Yaani mukiwa, .!watu wa namna hiyo ya imani basi shikamaneni

Siyo kushikamana tu ki ovyo ovyo;- *No where for nothing*.Kushikamana bi hablillaah – Na .!kamba ya Mwenyezi Mungu

!Kisha tunaambiwa baada ya kushikamana – Walaa tafarraquu, Musitafautiane

Hili la kuliandika aya hii linatuaonyesha wazi kuwa waandaaji wa semina hii, wakati .wakiandaa walikuwa na lengo la kutafuta mambo ya kuwafanya waislamu washikamanie

Yote tutakayoyazungumza, huja zitakazo kuwepo kwenye hadithi za Mtume (S.A.W), .lazima zilenge kwenye mshikamano wa Uislamu
Kwa sababu hili ndilo lengo muhimu kwa waislamu,hili la kushikamana. Kushikamana na kamba hii, ambayo ni dini ya Mwenyezi Mungu kama alivyoashiria mheshimwa rais kaika hotuba yake.

Kushikamana na dini ya Mwenyezi Mungu yenye meno mawili. Kama kamba yenye meno mawili imara. Kitabu LLaah na Sunatu Rasuulih Swallallaahu alaihi wa sallam; dini ya .Uislamu

Ikiwa kamba, basi dini ya kiislamu ni kamba yenye meno mawili matukufu.Meno yale mawili ambayo wajuzi wa uislamu katika kutuzungumzia wanatuambia haifai sisi kupotea wala kuwa gizani, madam tuna nuru hizo mbili; Qur'an na Suna ya Mtume Swallallaahu .alaihi wa sallam

Mtoa mada kufika hapo akasoma beti za mashairi za Ahmad Shauqi. Wakati akiendelea na .beti akaletewa kikaratasi. Halafu akasema kuhusiana na kikaratasi kile

Ningependa kuwahakikishia sekretariati kuwa mimi sototoa kwenye maudhui wala .sijatoka. Sasa vijikaratasi kama hivi ndivyo vitakavyonitoa kwenye amaudhui
Ningependa kuwahakikishia sekretariati kuwa mimi sitatoka kwenye maudhui wala .sijatoka.Sasa vijikaratasi kama hivi ndivyo vitakavyonitoa kwenye maudhui
Ningependa nipewe utulivu wa kuzungumza. Naliomba hili kutoka kwa *Chairman* na .kutoka kwenu nyote

Kuonekana kwa mwezi twashikana tunapokosana. Sisi na wale tunaokosana ni kuwa mwezi lazima kila pahala uonekane. Na au mwezi ukionekana sehemu moja kunawapasa .watu wa mahala pengine kufunga

Wakiuona watu wa mashariki, itawapasa na watu wa magharibi kufunga, au ni lazima na .?wao wauone kwa namna yao?,kwa sababu wana mji wao

Masuala ya kuthubutu mwezi wa Ramadhani, kufunga na kufungua, sisi tumeyahakikisha sote kwa pamoja. Tunashikana na tunaopingana nao, kuwa mwezi sisi hutujilia kwa njia .mbili

Njia ya kwanza ni kuuona mwezi, na njia ya pili ni kuambiwa mwezi umeonekana. Na hili likifaa kwa watu wa mji wa mbali na mji wa mbali. Vivyo hivyo kwa watu wa mji wa karibu na mji wa karibu. Bali na watu wa mji mmoja vile vile. Mwezi hutufikia kwa kuuona na kwa kuambiwa.

Hata watu wa mji mmoja si wote wanaotoka wakauona mwezi. Wengi wao ni wale wanaoambiwa tu kuwa mwezi umeonekana.Hata wale wanaotoka na vigoma kuwa wanakwenda kuuangalia mwezi hawauoni wote. Wanaounona ni wengine na wengine .huambiwa tu kuwa umeonekana

Tena mwenye kufurahika kiislamu na mwenye kufurahika visivyo kiislamu hufurahi pamoja. Lakini hawasemi mimi siondoki hapa wala siahidi kufunga mpaka na mimi .!niuone, hakuna

Sasa mwezi hutufika kwa njia mbili; kwa kuuona na kwa kuambiwa. Masuala ya kuona mwezi yamethubutu kwenye hadithi yamtume Swallallaahu alaihi wa sallam alipotuambia "Swuumuu Liru'yatih wa afttiruu Liru'yatih Fain ghumma alaykum, fa akmiluu iddata thalathiin". Fungeni kwa kuuona mwezi na fungueni kwa kuuona mwezi. Mkifinikiwa .kiwingu timizeni hesabu ya thalathini. Hili lina thibitisha kuuona mwezi

Njia ya pili ni ya kupewa habari kwa hadithi iliyopokelewa na Ibnu Abbas kwamba mwarabu mmoja mbedui ……;. Nataka patafautishwe na waliohudhuria hapa, baina ya .muarabu mbedui na mwarabu muarabu

Kiarabu yazungumzwa hivi;- A-arabiyu; muarabu nje ya miji ya Ustaarabu, Arabiyu; .muarabu wa mjini; A-arabun; waarabu wa mjini wenye kujua mambo yote

Ndipo Mwenyezi Mungu akasema katika Qur'an (9:97) (*MABEDUI WAMEZIDI SANA KATIKA UKAFIRI NA UNAFIKI, NA WAMEELEKEA ZAIDI KUTOJUA MIPAKA YA .(ALIYOYATEREMSHA MWENYEZI MUNGU JUU YA MTUME WAKE*

Watu wengine wengine wakaichukulia aya hii kuwa ni matukano kwa waarabu wote, kuwa .waarabu ni wanafiki mno. Sivyo mambo yalivyo

Sasa!alikuja huyu muarabu mbedui, anayeitwa (Aa-arabun, akasema Yaa rasulallaah mimi nimeuona mwezi. Mtume akamwambia *Atash-hadu anlaailaaha illa llaah?)* Wakubali kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja, hakuna Mungu mwengine ila yeye Allah?. Mwarabu akasema ndio. Mtume akamwambia Atash-had anna Muhammada rasuulallah?. Mwarabu akajibu ndio. Hapo Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam akamwamrisha Bilal awaambie .watu fungani

Kwake yeye Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam umethubutu mwezi kwa kuwa kaja .mwarabu tu kamwambia kuwa mie mwezi nimeuona

Hoja ya pili ya kuthibitisha kufunga kwa kupewa habari ya mwezi ni hadithi ya Ibnu Umeyr ya kuja msafara mzima. Pale ni mtu mmoja mwarabu, hapa ni kuja msafara mzima. Ulipokuja msafara ukamthibitishia Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam kuwa sisi tumeuona mwezi. Tenea msafara huu ulikuja mwishoni mwa mchana. Haukuja asubuhi .wala alfajiri

Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam akaamrisha watu wafungue. Tena ni mwisho mwa .mchana, wafungue na waswali Idi kesho yake. Hadithi hizi zinajulikana na wanachuoni

Hadithi nyingine ni ya Ibnu Umar (R.A): mtoto wa Umar Ibnu Khattab. Asema watu walikwenda kuuona mwezi. Mimi nikauona, nikampa habari Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam nikamwambia mimi nimeuona. Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam akafunga na .akaamrisha wegine kufunga

Sasa, haya ni yale mambo mawili niliyoyazungumza kuhusu kwamba mwezi huthubutu .kwa mambo mawili, kwa mtu kuuona na kwa kupewa habari kuwa mwezi umeonekana

Katika Qura'an tukufu, aya ambayo kwamba inayozungumzia kuuona mwezi au kuuhudhuria mwezi, anaposema Mwenzi Mungu Subhaanahu wa Taala (2:185): (*Mwezi huo mlioambiwa mfunge) ni mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika (mwezi) huo hii Qur'an ili iwe uwongozi kwa watu, na hoja zilizo wazi za uongozi na upambanuzi (wa baina ya haki na batili). Atakayekuwa katika mji katika huu mwezi (wa Ramadhani) *…… afunge*

Mwenye kuuhudhuria mwezi miongoni mwenu nyinyi, akawa yupo mwezi wa Ramadhani .ukija, akawa hana limzuialo kufunga basi aufunge huo mwezi

Sisi msimamo wetu ni kwamba mwezi unaozungumziwa hapa ni mwezi ule wa siku; mwezi mosi, mwezi 3, mwezi kumi, mwezi 15 mpaka mwezi ishirini na tisia au thalathini. Si mwezi ule *newmoon.* Haukusudiwi *newmoon*. Huja zetu hapa ni kwamba Mwenyezi Mungu hakusema*) Faman Shahida minkum L-hilaala; Faman raa minkum L-hilaala.* *.Amesema *Faman shahida minkum L-sshahara*

.*Tafsir ya Qur'an ya Skh Abdulah Saleh Farsy*

Mwenye kuuhudhuria mwezi miongoni mwenu nyinyi. Na dalili ipo kwenye aya yenyewe, aliposema *Falyaswumhu*, na afunge huo mwezi. Mwenyezi Mungu hawezi kutwambia na aufunge huo mwezi mwandamo.Mwezi mwandamo haufungwi, kama ingekuwa mwezi mwandamo wafungwa basi tungekuwa twafunga siku moja tu. Falyaswumh na aufunge .huo mwezi unaoitwa Shahar

Kwa hivyo hapana kuuona mwezi mwandamo.Na Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam tukishika mwongozo wa hadithi zake, twapata ya kwaba makusudiwa ya kushuhudia mwezi ni kuwepo kwenye mji. Kwa sababu Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam amesema kwenye hadithi moja *Liyubaligh Shaahidun minkum lighaaiba*. Aliekuwa yupo hapa amfikishie aliyekuwa hayupo *As-shaahidu hunaa bimaanaAl-haadhiru wa laisa .bimaana raaiy al-ladhiy yuraaa. Wa hadithul aakhir yuth-bitu haadhihi nuqta*

Pale Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam aliposema mwanamke asifunge funga ya suna na hali mumewe yupo mjini, akamuharibia kukaa naye, akamkosesha kufanya analotaka

kufanya naye kama mkewe. Mwanamke asiinuke tu akajifungia. Mumewe akija-Nana .vipi?; amwambiye mie nafunga!.Mtume hataki hivyo

Kwa hivyo hujja tuliyonayo hapa ni *Laa tasumanna mraatun wa baaluha shaahidun, ayyi .haadhiru*. Ndiyo makusudiwa tunayoyataka

.Kwa hivyo *As-shuhud ni bimaana L-hudhuur*.Ni kuwepo si kuona

Kwa hivyo baada ya kuyasema haya tuliyoyasema, sisi tuliohudhuria tuna misimamo miwili vichwani mwetu. Tunayo misimamo hii tulivyo nayo. Pengine mtu ana msimamo hayuko tayari kuuwacha msimamo wake AT ANY COST; na wengine tuna msimamo, .lakini tuko tayari tukipata hujja za sawasawa, tukamfuata mwengine mwenye hujja

Uzuri mtu awe na msimamo, lakini awe yuko tayari akidhihirikiwa na hujja za kisawa aseme mimi niko tayari. Attanaazulu Lil haqi Fauli Laah. Kuifuata haki ndio bora. Sio .kufanya ushindanishi na kupingana

Kitu kimoja kabla sijaenda mbele. Napenda kuwatanabahisha ndugu zangu. Sisi sote tutakayo kujazungumza hapa, tusijitie ufahali na uhodari mkubwa. Yote tutakayo kuyazungumza sisi hapa yashazungumzwa. Wanavyuoni bora kuliko sisi .washayazungumza

Wameyazungumza kama tutakavyokuyazungumza. Pengine kwa uzuri zaidi. Pengine kwa "*Circumstance*s zao". Kwa hali zao na wakati wao, pengine tu watakuwa waliyazungumza kivyao. Na sisi tunayaleta hapa ili tuyazungumze mbele ya ndugu zetu kivyetu. Lakini .hatutafanya jambo ambalo eti bado halijafanywa

Attamathalu hunaa bi qauli man qaala fiy bayti shiiri lahu. Walasnaa walau kun-na zawi hattabin yawmaan alal ahttaabin nat-tahidhu. Nabniy kamaa kaanat awaailuna. Tabniy. .Wa-naf'alu bimithli maa faaluu

Hatukuwa sisi, hata kama tungekuwa na vizazi vizuri, siku moja kwamba sisi tutakwenda kutegemea vizazi vyetu. Tutategemea amali zetu kwa hivyo tuogope Mungu. Tunajenga .kama walivyojenga waliotangulia. Na tunafanya kama walivyofanya wao

Tusijitie ufahari sana, tukajiona twaleta mapya mno. Laa!, haya yashazungumzwa. Sasa maukifi mawili haya ambayo sisi tunayo. Maukifi ya mwanzo – *Luzuumu ru'yat ahlu baladin swauma jami-i ahlul baladi.* Kulazimu kulazimisha watu wa mji fulani kufunga watu wa miji yote ulimwenguni. Msimamo wa pili, kutolazimu kuuona watu wa mji .kufunga watu wa miji yote. Pawe na wao kuuona kwao

Wenye msimamo huu wasema la! msimamo huu ni makosa.Na wenye msimamo huu wasema la msimamo huu ni makosa. Na ndipo pakapatikana ikhtilafu; na ikhtilafu .haziwezi kutuepuka

Sababu sisi tumeumbwa tukhtilafiane. Katika Qur'an Mwenyezi Mungu amesema *Walidhaalika khalaqahu.* Wameumbwa kwa ajili ya huko kutafautisha. Watakhitalafiana tu. Kuteta na kutopatana ni bidhaa alifungamaniwa. Adam alipotoka peponi, yeye na Hawaa . *Baadhukum Libaadh aduwun,walakum fil-ardhi mustaqarun wa mataaun ilaa hiin-.Qur-2:36. Ihbituu minhaa jamian-.Qur-2:38*

Kuteta tutateta tu, lakini sasa yategemea utateta na lipi, ulitetee lipi?. Lakini kuteta tutateta tu. Utateta na haki uitetee baatili, au utateta na baatili uitetee haki. Utakata shauri weeye, .lakini kuteta kuko

Tutateta umri wetu wote mpaka tutoke hapa duniani. Waliteta waliotangulia na sisi twateta na watakaokuja watete. Tutahesabiwa tulitetaje na tuliteta kwanini, na tulitetea nini. Lakini .kuteta kuko, hakutuepuki

Kwa hivyo tuliambiwa, lakini mukipatikana na jambo la kuteta mutafanya nini?, ni kufuatwa *hamalan.* Inna Rasuula Swalla-Llwaahu alaihi wasa-sallam, wa huwa saadiqul masduq unzilat alayhi aayatun, taquulu- *Alyawma akmaltu lakum diinakum, wa atmamtu .alaykum niimatiy, waradhiitu lakumu- L- islaama diina-Qur-5:3*

Mtume kateremshiwa aya hii, ya kwamba dini nimekukamilishieni, na neema ya Mwenyezi .Mungu nimeitimiza. Hakutuacha hamalan, hakutuacha kama kondoo wasio na mchungaji

Kila kitu alitwambia, na kila kitu alitu-tanabahisha. Hamuna namana ila mutete. Sasa .?mukiteta mutafanyaje

Tulipewa neema, yakija mambo ya utesi. Yakija mabo ya vuta nikuvute mwanangu. Huyu .?avuta huku na yule avutia kule tutaamuliana na nini

Mwenyezi Mungu asema (4:59): *Fain tanazaatum fiy shay-i farudduuhu-i-laa Llaahi wa rrasuuli……. Mukiteta, mukitafautiana katika jambo lirejesheni kwa Mungu na Mtume* .Swallallaahu alaihi wa sallam

Na sisi hapa tupo mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam . Kwa sababu Qura'n ipo na suna za Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam zipo. Ndipo tukaambiwa kwenye khutba ya ufunguzi, tuishi kwenye muongozo huu wa Qur'an na .hadithi za Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam

Tuwache ujabari wetu, wa kuzipiga teke aya za Mwenyezi Mungu na kuzipa mango dhikri za Mtume Swallallaahu alaihi wa sallam . Tusije tukenda tukafufuliwa vipofu kisha tukatoa hoja (20:124). *Wa man a-aradha an dhikry. Fain-na laahu maishata n dhankan .wanahshuruhu yawma L-qiyama a-amaa*

Qaala Rabiy Lima hashartaniy a-amaa waqad kuntu basyiiran. (20:126) *Qaala* .(20:125) *.kadhaalika atatka aayatunaa fanasii tahaa. wakadhaalika L-yawma tun-saa*

Mwenye kuupa mango utajo wangu, wafasiri wanasema utajo ni utajo wa Mwenyezi Mungu na ni AlQur'an waraasuulu Swalla Llaahu alaihi wa sallam

Kwa hivyo tusiupe mango mafunzo za Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam, tukang'ang'ania fikra zetu, upendo wetu na hawaa zetu za kibinafsi na kwamba mambo .haya tumeyazoea tangu zamani

Uislamu ulipokuja, jambo lake muhimu ilikuwa ni kuwaondoa watu kwenye jambo walilolizoeya kuwapeleka kwenye ambalo hawakulizoeya.Kwenye waliloliozoeya wanalolipenda kuwapeleka kwenye ambalo hawakulizoeya wasilo lipenda. Hili ndilo ..jambo muhimu ambalo kwamba Uislamu ulikuja kulifanya

Kwa hiyo sisi tukiitwa kweye jambo, na ikawa hatukulizoea, tukasema aah! Lakini haya ni mapya na sisi, itakuwa imani bado haituvuti kwa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam , .na yataka ituvute

Sasa tuone hoja za kwamba ukionekana mwezi kwenye mji, huwalazimu watu wa .ulimwengu mzima wafunge

Awalan, qauluhu swalla llaahu alaihi wa sallam. Kutokana na mafunzo ya Qur'an .tumefaradhiwa kuufunga mwezi wa Ramadhani

Ndugu zetu mahala Fulani wameuona mwezi, wakishauona mwezi wa Ramadhani umeandama huwa pamekuwaje hasa?. Huwa pamekuwa Ramadhani imekuja. Naam!, ndugu zetu waislamu wanaoshuhudia Laa ilaaha illa Llaah, wa Anna Muhammadan .! Rasuulu Llaah wamesema wameuona mwezi, ni kuwa Ramadhani ishakuja

Ni wajibu wa kila muislamu popote pale alipo, ikiwa mwezi wa Ramadhani umefika na siku hizo zimefaa kuitwa ni siku za Ramadhani, ni lazima afunge. Akitofunga siku moja .bila ya ugonjwa wala ruhusa ya kutofunga, basi siku hiyo hawezi kuilipa maisha yake yote

Kitu kingine ni hadithi ya Mtume isemayo *swuumuu Liru'yatih wa affttiruu Liru'yatih*. .Fungeni kwa kuuona mwezi na fungueni kwa kuuona mwezi

Amri hii inatuhusu sote waislamu. Haiwahusu watu wa mji ikawa watu wa mji mwengine haiwahusu. Ni waislamu wote waamrishwa kwa pamoja wafunge kwa kuuona mwezi. Na .jambo la kwamba kila mmoja lazima auone mwezi tulikwisha kulizungumza

Kuna bwana mmoja alilitolea shub'ha hili, akisema, tumeamrishwa kufunga, lakini kila mtu atafunga kwao utakapoonekana. Hilo halina shazi, halithibitishi ulazima kuwa mwezi ukionekana mahala kuwa watu wa miji yote wafunge. Huoni sote tumeamrishwa kuhiji, lakini tukienda Makka, watu wengine miiqati yao ni Dhul hulaifa, wengine ni wapi, na .!wapi

Hayo ni maneno ambayo hayastahiki hata kuzungumzwa. Lakini nimependa kuwatanabahisha baadhi ya ndugu zetu. Hata *miiqatu* ni *makaani* kwanza. Halafu Mtume

Swalla Llaahu alaihi wa sallam alipotaka watu watafautiane katika hizi miiqati za kimahala, alibaini, hakutuwacha. Na katika hili la kufunga Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam angebaini kuwa kila watu wasubiri wauone mwezi kwao. Hivyo hilo na hili halifanani. Kwa sababu hata kama yafanana, lakini hili pana ufafanuzi wa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam

Kitu kingine, siyasa ya sharia ya kiislamu, Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam anataka kutukutanisha na kutuweka pamoja katika kumuabudu Mwenyezi Mungu – *Wa iyyaaya faa buduuniy*. Kwa hivyo kama ilivyokuwa hiyo ndiyo siyasa ya Mtume Swalla Llaahu alaihi .wa sallam; siyasa ya sharia- *Al siyasa Al amma al-tashriik;* ni kutufanya sisi kitu kimoja

Na sisi twaliunga mkono hilo kwa asasi zetu ambazo kwamba zimetusukuma mpaka .tukaweka semina hii

Tumepaswawa na kwamba sisi twatafautiana tufanye ibada zetu kwa pamoja, kwa mtindo .mmoja. Ni kwamba ni mfumo wa hata sala zetu

Tumewekewa maneno fulani, ndio tunayoyasema katika sala zetu. Pahala popote utakapokwenda sala inasaliwa sampuli hiyo hiyo moja. Sote tuna wajibu wa kuisoma fatiha katika sala. Huwezi kukuta mahali kwamba watu wengine wakiswali wasema hivi na .wengine wasome vile

Watu wote wasoma fatiha. Wakirukuu, wakisujudu wasema maneno mamoja. Ni kwa sababu tumetakiwa sisi tushikanishwe na tuwepo mahali pamoja. Na hili sikulisema tu kwa .fikra

Tunatakiwa tufunge kwa siku moja, tufungue siku moja na tuchinje siku moja. Ni haki gani waislamu sisi tujifanye ni vichekesho kwa wasiokuwa waislamu. " Nyinyi mumefunga leo?", "Ah!, sisi shehe letu ni fualani tutafunga kesho kutwa sisi". Twachekwa na watu wa .dini nyenginezo, na hali hatukuwa na sababu ya kuchekwa. Sisi – *Al islaam Nadhiif*

Dinun Nadhiif, Dinul haqu, kwa nini iwe ni kichekesho, dini ya kuchekewa. Dini ya kiislamu tukufu, tohara. Dini iliyoletewa kwa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam . Anaambiwa *khairul An-biyaau walmursaliina.*Kwa nini tuitoe mbele za watu, tuwape watu .nafasi ya kutucheka sisi kwenye dini yetu

Wengine wafunga Jumapili, wengine Jumatatu, wengine watafunga Jumanne. Wengine .?hawajafunga wengine wanaswali Idi, wengine hawajaswali, kwa nini iwe hivyo

Hadithi ya Aisha (R.A); *Al-fitru yawma yufttiruuna Nnaasi, Wal adh-haa yawma yudha hiina Nnaasi*. Yaani zote zaelekea kwenye mwelekeo wa kwamba, mambo haya ya .kufunga na kufanya *Udh-hiya* tuyafanye siku moja. Tuwafikane tuyafanye siku moja Sasa baada ya kuzungumza haya *Umuuman* ningependa nizitulize nyoyo za baadhi ya ndugu zetu, ambao kwamba pengine waonelea kwamba twayazungumze haya kiupya upya. Hatuzungumzi kiupya upya, twayazungumza haya kama yalivyokuja katika vitabu vya .kiislamu tunavyovijua na tunavyovikubali

Na nimeandika maneno kutoka katika vitabu vinane. Inshaa Allahu taala kutakuwa na utulivu nisome yaliyo katika vitabu, kisha nitoe taaliq yangu. Kisha huo utakuwa ndio .mwisho wa takdiim yangu ya mada hii ya *Al-luzuumi wa Addamu L-luzuumi*

Kwanza AL MUGHNIY-Kitabul Mughni cha Ibnu Qudaama, na kitabu kipo hapa, ningependelea chairman aniruhusu nimuombe mtu akitoe pale, Bwana Majid simama, unitolee kimoja kimoja, ukifunue, atakayekwambia nataka kukisoma umpelekee. Bwana Majid akasimama.

Al-mughniy juzuu ya 3.Chapa ya bwana Majid yaweza kuwa tofauti na chapa ya kwangu. *Idhaa raa-a L-hilaala ahlul baladin lazimma jamia-nh bilaadi swaumu*, Wakiuona mwezi watu wa mji fulani, huwalazimu watu wa miji yote kufunga. Hiyo hoja yetu ya kwanza kwenye kitabu Al Mughniy cha Ibnu Qudaama.

Kisha Mughniy ameeleza kuwa hili neno la Laz ni neno la baadhi ya watu wa Shafii na baadhi yao wamesema kuwa, ikiwa baina ya mji na mji kuna masafa marefu, kwa hivyo itawalazimu kila watu wa mji wauone wao wenyewe. Kisha anasema *Wa inkaana baina humaa buudun*. Ikiwa baina ya mji na mji kuna umbali. Ikiwa hakuna umbali basi watafunga pamoja. Kisha akatoa mfano pale Iraq na Hijaz, na Sham na Shami. Basi kila watu wa mji watategemea kuuona kwao.

Sasa mimi hapa! Kwenye hoja hii nataka kuwatanabahisha jambo moja. Tumeambiwa kuwa miji ambayo iko mbali mbali --------, kwenye vitabu vya fiqh; ambayo ni ya kufunga mbali mbali ni kama ya Iraq na Hiza. Jee hivi leo Iraq na Hijaz wafunga mbalimbali?. Musinijibu, jibuni kwa vichwa vyenu wenyeewe.

Sham ni Syria; jee Syria na Hijaz wafunga mbali mbali? kwa sababu mat-lai zao zatafautiana?. Kwa hivyo hayo ni mambo ambayo ni "*Out dated*" hayapo.

Kitabu cha pili ni FIQHU SUNNA cha Said Saabiq. Ni kitabu maarufu chajulikana na watu wote. Ameweka mlango kamili kuhusu tatizo la *Ikhtilaaful mattaali'i*.
Asema Said Saabiq*: Dhahaba L-jamhuur* ; Mkao mkubwa wa wanavyuoni wamesimama msimamo wa kuwa *Laa Ibrata Li-ikhtilaafI Al mattaali-i*; Hakuna mazingatiwa ya kutafautiana matlai, hakuna mazingatiwa ya kutafautiana matlai.

Anasema, Popote, watu wa mji fulani wakiuona mwezi, hupasa kufunga watu wa miji yote kwa kauli ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam, *swuumuu liru'yatih wa huwa .khittabu L-Aamu*; na ni ADDRESS iliyo wazi yaliyoelekezwa umma wote wa kiislamu

Mwenye kuuona mwezi katika hao waislamu walioambiwa *Swuumu Li ru'yatih* basi mahali popote. Huku huwa ni kuuona wote. Kwa sababu jambo lao ni moja wote, moja .!wote

.Kitabu cha tatu cha **AL MIIZAAN** cha Abul Wahab Shiirami

Marehemu Sheikh Ameir Tajo akaingilia kati, akitaka mtoa mada asome katika kitabu hicho (cha FIQHU SUNNA) na hoja za upande wao. Mwenyekiti akawa anampelekea kitabu. Lakini mwenyewe; Skh Ahmad Muhammad Msallam akajitetea kwa kusema " Sheikh Kasahau kuwa sisi twasoma hoja za upande mmoja tu; wa kwetu" Mwenyekiti wa semina akasuluhisha kwa kusema " Si kuna kuchangia! Huyu bwana anaeleza hoja zake, kisha yule ambaye ana hoja zaidi ya hizi atazieleta. Uwanja ndio huu, na farasi leo ndio ."yupo hapa
Baada ya Skh Ahmad Zubeir kusema hayo, mtoa mada akaendelea; Kabla sijasema, napenda tuyajadili haya kwa udugu, kufuatia ule ule mwongozo wa msheshimiwa rais, .kuwa hatuteti, twafahamishana, na tunasaidiana kufikilia kwenye haki

Juzuu ya 2 Saf-ha ya 9 ya Al Miizaan. Asema mwenye Miizani Wattafaqu alaa annahu idhaa ruuiya L-hilaala fiy baldatin qaasiyatin Annahu yajib swaum alaa jami-i ahli diyaari. .Illa anna as-haaba shaaf-iy ikh-talafu fiy dhaalika

Wameafikana wanavyuoni ya kwamba mwezi ukionekana katika mji Fulani wa mbali, huwapasa kufunga watu wa mij yote mingine. Wote wameafikana isipokuwa baadhi ya wafuasi wa imamu Shaafiy wameona tofauti ya matlai. Nani walio-ona? Ni baadhi ya .wafuasi wa imamu Shaafiy. Hajatajwa imamu Shaafi mwenyewe

Kuna tofauti wasomi!. Wale munaosoma vitabu nyie. Kuna tofauti baina ya kuambiwa katika vitabu vya fiqh, Qaala shaafi-iya na Qaala Shaafi-iyu .Qaala Shaafi-iya ni wafuasi wa imamu Shaafi; wanaojisema wanafuata madh-hebu ya imamu Shafii. Hawa Sahaafi-iya pengine wanasema maneno ambayo imamu Shaafi mwenyewe hakuyasema.

Kitabu cha nne – **ALFIQHU ALAA L-MADHAAHI-BIL-L-ARBAA,** mujaladi ya 1, Fiqhul-ibadaat uk.550 ikiwa chapa zinaafikana. Daarulfikri-Beirut cha kwangu. *Idhaa .thabat ru'uyat L-hilaala bi kusrin minal aksaar wajaba swaumu alaa saairul aksaar*

Wala hapana cha umiji. Kwa mfano Namanga ya Tanzania ifunge na Dodoma, na Namanga ya Kenya ifunge na Aamu. Hakuna cha umiji, ni mwezi kuonekana na .kutoonekana

Kwa hivyo; asema huyu: Laa farqa baina L-qariibi min jihatil thubuut idhaa balaghahu wal baiidi min jihati dhaalik, idhaa balaghahu min taariq bi muujibi-l-swaumu. Walaa ibrata Li-ikhtilaafil – mataali'i.

!Hakuna mazingatiwa ya kukhtilfiana mataalii. Nukta hamna

Nataka kuwatanabahisha wasomi kwenye nukta moja hapa. Tumekuwa twakariri sisi jambo la matlai; kutofautiana matlai na kutotafautiana. Wasomi nyinyi!. Mumejiuliza hata mara moja, kwamba mwezi hauna kitu kinachoitwa matlai

Laisa Lil-qamari shaaiun yuqaalu lahu matlai. Inna LLaaha subhaanahu wataala lam yushir ilaa matlai L-qamar fil qura'anil kariim. Inna maa tahadatha an matlai L-shamsi.

Inna an-zalnaahu fiy Lailatul qadri……salaamun hiyya hata mattlai L-fajr.

Haikuambiwa matlail qamar. Matlail fajr hutokea kwa kutokea jua au kwa kuanza jua kutokea, au kwa kukurubia jua kutokea. Kwa hivyo ni matlai L shams.Hakuna kitu kinachoitwa matlai L hilaali

Lil-hilaali manzilun mina Lmanaazili. Lahu manaazilun wal buruuji.

Naquulu-*Walqamaru qadar-naahu mannaazila.Famin ayna lahu ikhtilaafu lil mataali'i L-qamaru, wa min ayna lahu dhikrun Li matlai L-qamari. Min ayna*?.

.....!Kitu Kingine

Kabla mtoa mada hajaendelea kulikuwa na mkono umenyooshwa, mtu alitaka kuchangia. Mwenyekiti akakatisha kwa kukataza watu kuinua mikono wakati mtoa mada akiendelea na mada yake. Mwenye kutoa mada akasema yeye hawezi kumzuia mtu kufanya hivyo, .akasema:Ndio hali mtu akipenda jambo mno, la uislamu

Kitabu kingine ni AL-UMMU cha imamu Shaafi, mujaladi ya 2 uk 94. Hapa nataka nieleze kwamba, tumekwenda kuyatafuta maneno ya imamu Shaafi mwenyewe. Asemaje na asema wapi. Tukapata kitabu ambacho ni cha Imamu Shaafi mwenyewe,kinaitwa **Al-Ummu**

Kwenye kitabu hiki, imamu Shaafi alipozungumzia habari ya mwezi, ametaja hivi, kwenye kufasiri hadithi iliyopokewa na Ibnu Omar (R.A), akasema: *As-sha haru tis-un wa ishiruuna. Laa taswuumuuu hataa tarauhu L-hilaala, wa laa tuf-ttiruu hata tarauhu. Fa in ghumma alaykum fa akmilu L-iddata thalathiin.Qaala Shaafi iyu; Fa in lam tara ammatu hilaala shahari Ramadhani.Wa ra ahu rajlu aqlun . Raaitu An aqbalahu Lil athar wal ishtiyaqu.*

Imamu Sahaafi amesema, ikiwa watu wote hawakuuonana mwezi wa Ramadhani na akauona mtu mmoja muadilifu. Naonelea niikubali hivyo. Kwa sababu hadithi ya Mtume .Swalla Llaahu alaihi wa sallam yaelekeza hivyo, na kwa sababu ya kutoka shakani

Haya ndiyo maneno ya imamu Shaafi mwenyewe kuhusu mwezi. Imamu Shaafi akubali maneno ya mtu mmoja tu. Al-imamu Subqiy ametanabaihisha, na mwengine amemfuata :Subqiy asema

.Alaa annahu yalzamu mina Ru'ya fil baladi sharqiy ru'yatahu fil baladi gharbiy

Hulazimu kuuona katika mji, ulioko mashariki, uwe umeonekana katika mji ulioko .magharibi

Hapa mimi lengo langu ni moja tu katika maneno ya Subqiy. Nataka niwatanabahishe namna wanavyuoni wetu walivyokuwa wakialili hoja. Saa nyengine *Yusbihu taalilu i-*

ilaalan badalan an yakuuna taalila. Mara nyengime huwa ni katika kuleta uhondo tu wa ile hoja, badala ya kuwa ile hoja ndiyo hoja yenyewe.

Idh Lailu yadkhulu fil bilaadi sharqiya qabla. Wa qadhiyatu kalaamihim annahu mataa .ruiya fiy sharqiy laazima kullan qharbiy bi nisbat sharqiy alaa amal

Kwa sababu usiku huingia katika miji ya mashariki kwanza. Na maneno yao ukisha kuonekana kwa watu wa mashariki lazima na watu wa Magharibi nao waambiwa wameuona. Na si kinyume na hivyo.

Na ilivyo ni kwamba watu wa magharibi wakiuona mwezi. Watu wa upande wa mashariki .itakuwa imehakikisha kuwa watu wa mashariki wameuona mbele zaidi

Kwa-nini wakiuona watu wa mashariki iwapase watu wa magharibi. Wakiuona watu wa magharibi ambao ndio wanaochelewa kuona na isiwapase watu wa mashariki. Hicho .nakiona ni kama n'kinyume

.Kitabu **AL AFNAANU NAADIYA**; **sherh subuli sawiya li fiqhi sunanil mar wayya**

Amesema masuala haya watu wametafautiana. *Dhahaba alfuqahaau kal Qassim bin Muhammad. Anna likulli ahli baladi ru'yatahu*; Kuna kila watu wa miji wana kuuona kwao.

Hilo amelitaja Tirmidhiy kutoka kwa watu wa elimu. *Walam yahkiy siwaahu* Wala hakulitaja na mwengine aliyelieleza asiye kuwa Tirmidhiy.

Wa tadalla haau laai.Hawa wamechukua dalili *Bimaa rawaahu Ahmad* kwa alilo lipokea Ahmad, wa Muslim wa Tirmidhiy an Kuraib kutokana na hadithi ya kuraib iliyo .mashuhuri

Wadhahaba Jumhuuri L-fuqahau illa anaahu idhaa ruiya –hilaalu. Jamhuri ya wanavyuoni wa fiqhi wamekwenda ya kwamba ukionekana mwezi katika mji lazima; *ahla L-bilaada kullahaa an yaswuumuu*. Inawapasa watu wa miji yote wafunge ummuu) inawapasa watu wa miji yote wafunge. *Li anna khittaba qauli rasuuli Laah swalla llaahu alaih wa sallam; swuumuuu Liru'yatih khittaabu aammman*. Kama tulivyoona huko nyuma. Kwa sababu maneno aliyoyasema Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam kuwaambia waislamu wote.

Wa Li anna Ramadhaan; Na kwa sababu Ramadhani *thabatat kulluhu*; ishathubutu kuingia kwake. *Fathabatat ahkaamuhu.* Kwa hivyo hukumu zake zithubutu. *Fathabatat swiyaamuhu alaa umumi L-muslimiina*. Kwa hivyo ishathubutu kufunga mwezi wa Ramadhani juu ya waislamu wote. *Bi ru'yat adlun minhum fiy ayyi makaani*. Kwa kuuona muadilifu miongoni mwa waislamu pahala popote.

Na uadilifu tukumbuke alioutaka Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam ni mtu kuamini *An-Laa ilaaha illa Llaahu wa anna Muhammadan Rasuulu Llaah*. Basi huyo ni *adlun* kama alivyotufundisha Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam .

Wafassala baadhul-fuqahaai; Baadhi ya wanavyuoni wamepambanua hapa, wakasema *Kashafi-iy;* kama imamu Shaafi; *Fiy L-mash-huriin An-hu*; katika kauli yake iliyo mashuhuri; *Wa haadhih nuqttatun ukhraa, qaulun mash-hurun an shaafi-iy; Laa yalzamu an yakuuna qaulan swahi-han mash-hurin an shaafi-iy.* Ni kauli mashuhuri mno kwamba imepokewa kutoka kwa Shaafi. *Wa haadha nahnu na-akhudhuhu.* Na hii tumeipokea kutoka kwa watu wa Shaafi.

Hakuna lenye kututhibitishia kuwa imamu Shaafi mwenyewe kasema hivyo. *Fa Qaala*;akasema; *In-khtalafat L-mattaali'i*. Matlai yakitafautiana; *Falikulli qawmin matt-lauhu*. Kwamba kula watu watafuata matlai yao.

Sasa, kuna na nukta nyengine. *Wahadh-aa siyaaghun Ibnu Taymiah*. Na Ibnu Taimiya kafuata msimamo huo, ya kwamba kila watu wawe na kuuona kwao.

Laa swiyaama Li ahli sharqiy L-aqswaa Walmaghribi L-aqswaa. Hasa hasa kwa watu wa FAR EAST NA FAR WEST, magharibi ya mbali na mashariki ya mbali, au mashariki ya .mbali na magharibi ya mbali. Hasa kwa hao. Ibnu Taimiya amechagua msimao huo

Na huu ndio msimamo wa Ahmad bin Hambal, na huu ndio msimao wa wanavyuoni wa .Saudi ;Arabia. Kwa hivyo kama mchango tu, wa kuwatanabahisha ndugu zetu

Watu wengine hudhania kwamba sisi msimamo huu twaletewa kutoka Saudi Arabia. Hatuletewei kutoka Saudi Arabia kwa sababu wanavyuoni wa Saudi Arabia wenyewe fat'wa yao ni kuwa kula mtu auone mwezi kwao. Sisi tunauchukua msimamo huu kutoka katika nususi za Qur'an na nususi za hadithi za Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam .Hatujali nani alisema au kuna nani walisema.
Mtu hatuondoshi kwa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam mpaka atusimamishe kwa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam .Huu ndio msimamo wetu.

Sasa! Kitabu kingine AN-NAWAWIY katika SHERH MUSLIM. Asema ameileta hadith ya Kuraib, ambayo kwamba yajulikana sana.

Kisha An-nawawiy amesema*; Waswahihun* Na lililo sahihi; *In – da ashaabinaa*; Lililo sahihi kwa watu wetu; *Anna ru'yata Laa taummu nnaasa*; Kwamba kuuona hakuwaenei watu wote*; Bal takhataswu Liman qaruba alaa masafa-h;*Bali linamuhusu yule ambaye kwamba masafa yake ni ya karibu na pale ulipoonekana mwezi.

Wa qaala ba-adhu as-haabinaa; Asema Nawawiy mwenyewe. Baadhi ya watu wetu, wafuasi wa imamu Shaafi wamesema; *Ta ummu ru'ya*; Huenea kuuona; *Li maudhi-yi*; kuonekana mahali*; jami-an ahlu L_ardh*; Huenea hukumu yake watu wa ardhi nzima; *Maf-huum*?

Shafi-iya wamegawanyika sehemu mbili. Baadhi wasema huenea, na baadhi wasema haienei. *Jamhuur*; msimamo mmoja kwamba hakuna *ikhtilaaful – mattali'i*. al-Hanaffiya msimamo mmoja. Al – Malikiy msimamo mmoja.

Li Shaafi-iy; Na wao wenyewe mashawaafiy hawako pamoja kwenye jambo hili. Wamegawanyika sehemu mbili.

KITAAB – NAILUL AWTAAR cha Shaukaniy, mujalad wa 2, juzuu ya 4, safha 194: .imeileta hadithi ya Kuraib

Baada ya kuieleza hadithi ya Kuraib amesema*; Wa qad khtalafa fiy dhaalika alaa madhaahiba;* Wamekhitalafiana katika hilo kwa madhehebu mengi. Baada ya kueleza tofauti zilizopo, wengine hulazimu, wengine hailazimu. Wengine hulazimu ikiwa masafa ni marefu, wengine hailazimu.

Kwa kifupi mwisho amesema; *Wa – a'alam*; Jua *Anna L- hujjata*; Kwamba hoja hapa; *Inna maa hiya*); Hakika hiyo huja; *fil marfui;* iko kwa lile lililopokelewa*; Min riwayyati Ibnu Abbas*;Miongoni mwa riwaya ya Ibnu Abbas*; Laa fiy Ijtihaadi.* Haiko hoja katika ijtihadi ya Ibni Abbas. Ibnu Abbas amesema ---------- Kwanza hadith iko hivi, ili tufahamiane.

Kuna bwana mmoja aitwa Kureb (Kuraib). Alikuwako Madina. Akatumwa Kureb na mwanamke aitwae ummul Fadhli. Akamtuma Shaam alipokuwako Muawiyya bin Abi .Sufiyani Amirul Muuminiina

Alipokwenda kule, akamaliza haja zake. Aliwacha mwezi umeoeanekana; Lailata Jum'aa; Akaja zake pole pole, Ikiwa ni kwa miguu, ni kwa ngamia, mpaka akafika Madina.

Akifika Madina Ramadhani tena ni mwisho wakazungumza na Ibnu Abbas.

.Ibnu Abbas akamwambia; Jee nyiyi mwezi muliouna lini nyinyi kule? Sham

Kureib akamwambia; sisi tuliuona *Lailata Jum'aa*. Ibnu Abbas akamwambia; sisi hapa tumeuona *Lailata Sabt.* Kwa hivyo tutaendelea kufunga mpaka tuuone, au tukamilishe .siku 30

Kureib akamwambia Ibnu Abbas; Al – laa taktafiy bi ru'yat Muawiyah? ; Hutosheki kwa .?kukwambia mimi kuwa Muawiya aliuona na akafunga, na watu wakafunga

Ibnu Abbas akamwambia*; Laa! Ha-kadhaa amaranaa Rasuulu LLaah;* Mtume ametufundisha hivyo.
Sasa! Ibnu Abbas hakutaja, Mtume alitufundisha hivi aliponena vipi, hakutaja!. Na hadithi .za Mtume ni nyingi

Hapa Ibnu Abbas *Sarahatan;* kwa uwazi hakutaja ni ipi hiyo hadithi ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam anayokusudia. Alisema; *Hakadhaa amaranaa rasuulu LLaah swala LLaahu alayh wasallam*.Lakini kuna dalili ya kwamba Ibnu Abbas aliikusudia hadithi fulani.

Aliposema Ibnu Abbas tutaendelea kufunga mpaka tuuone au tutuimize thalathini, twaweza kusema ya kwamba kuwa makusudiwa ya hadithi ya Mtume *swala LLaahu alayh wasallam* aliiyoielekeza hapa ni aliposema;*Swuumuu Liru'yatih waafttiruu liru'yatih, fain .ghumma alaykum fa akmiluu l-iddat thalathiin*

Twasema kwa kudhania pengine ni hadithi hii tukijenga juu ya hoja ya matendo ya matamko ya Ibnu Abbas mwenyewe. Basi hadithi hii yazungumza habari ya waislamu .wote kuuona mwezi. Hakuna habari ya watu hawa kuona na watu hawa kutokuuona

Jambo jengine! Tukizunguka katika vitabu vyote vya hadithi na fiqh, hatuwezi kupata popote neno la ikhtilaaful mattaali'i. Hatupati tukizunguka kwenye vitabu vyote vya fiqh na hadithi hatuwezi kuona neno la hujja lenye kutegemewa kwa Mtume *swala LLaahu alayh wasallam* linaloleta "PHRASE" HII; IBARA HII *Inna Likulli Baladin .Ru'yatuh*;Kula watu wana kuuona kwao

Maneno haya mawili ambayo watu wa upande mwengine wayashikilia; hakuna katika Qur'an. Hakuna kwenye hadithi za Mtume *swala LLaahu alayh wasallam* . Hakuna kwenye vitabu vya kutegemewa ambavyo kwamba vyachukua muongozo kutoka kwa . hadithi za Mtume *swala LLaahu alayh wasallam*

Hakuna kineno hiki cha "*Inna likulli Baladin Ru'yatuh*". Na wale ambao kwamba watachangia kinyume, wangefanya ihsani wakatwambia iko kwenye hadithi za Mtume *swala LLaahu alayh wasallam* . Wangefanya hivyo. I NEED THE CHALLENGE

.Kitu kingine! Hili haliwahusu watu wa upande huu na watu wa upande huu

Anazungumza Shaukany kwamba "*Fal istidlali bihi*" kutoa hujja kwa hadithi hii "*Alaa luzuumi ru'yati ahli baladin bighairihim*". Kulazimu kuuona watu wa miji kuwalazimu watu wengine wafunge.

Min ahli L-bilaadi adh-haru; Huja hii, hadithi hii ina nguvu zaidi ku*support* upande huu kuliko ; *minal istidlaali*; kuliko kuitolea dalili; *Alaa adami Luzuumi*; Juu ya kutokulazimu.

Hadithi hii hii ambayo kwamba watu waishikia hoja ya kwamba yathibitisha kutolazimu, mwenye kitabu hiki; Shaukany, asema yaunga upande ule wa kulazimu kuliko kuunga upande huu wa kutolazimu .

Kisha Shaukany amalizia maneno yake kwa kusema; *Al-ladhiy yanbaghiy it-timaduh*; Na lile ambalo kwamba lataka litegemewe; *Huwa maa dhahaba Al Maalikiyya*; Ni lile ambalo kwamba wamelithibitisha watu wa Malik.

Amezungumza mpaka akaja kwenye kineno cha kwamba*; wahakaahu Qurtubiy*; Na jambo hilo hilo Qurtubiy amelieleza; *An mashaaikhih*;Kutoka kwa masheikh zake; *An-nahu*; kwamba; *Idhaa ra-ahu ahlu baladin*; Wakiuona watu wa mji mwezi; *Laazima ahla bilaadi kullihaa*; Itawapasa watu wa miji yote wafunge.

Sasa natija ya maelezo haya yaliyotoka katika vitabu nilivyowatajia, na vitabu viko mbele yenu. Na hadith mumezisikia. Ni hivi:-

Kufupisha niliyoyazungumza. Tumeona kwenye maneno haya niliyowaeleza kwa kifupi ya kwamba kuna misimamo miwili.

Wa kwanza ni kulazimishia kuuona mwezi watu wa mji kufunga kwa miji yote. Pili kutolazimu kuonekana mwezi mahala kufunga watu wa mahali nyenginezo wasio kuuona mwezi.

Tumeeleza kwa kifupi kuwa huja za upande wenye kulazimisha wakiuona watu wa miji wafunge wa miji yote, ni hoja hizi zifuatazo. Ya kwanza ni kuenea tamko la hadithi ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam aliposema; *Swuumuuu*--; Fungeni nyinyi waislamu wote. *Al khittaabu aamun Lijamii – ilmuslimina*. Na hukukmu ya Khuttba kuenea *Lijamii – ilmuslimiina* inajulikana na wasomi wote.

Jambo la pili makusudio ya mfumo wa Sharia ya Kiislamu, ambao kwamba mfumo huo ni kuwa tanganya; ni kuwa kusanya umma juu ya msimamo mmoja.Yalenga juu ya hilo,kwamba tufunge siku moja na tufungue siku moja.

Tatu ni huja ya hadithi ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam aliyosema hapa, wazi wazi, kuwa fungani siku moja, mfungue siku moja, mfunge siku moja. Na kwanini, sisi wana wa mila moja tusifanye mambo yetu pamoja?.

Nne ni masua la ya Arafa;kusimama Arafa. Tumeambiwa na Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam *Swaumu Arafa yukafiru sanatain*, *maadhiya mustakbali*. Kufunga siku ya Arafa huondosha madhambi ya miaka miwili; mwaka uliopita na mwaka utakaokuja.

Mtu akifunga siku ya Arafa, ikawa ni siku ya Arafa ile aliyoifunga, basi madhambi ya mwaka uliopita na mwaka utakaokuja husamehewa.

Kwa hivyo kufunga siku ya Arafa ni muhimu sana. Lakini hatutostahili kupomoshewa madhambi ya miaka miwili; mwaka uliopita na mwaka utakaokuja; mpaka tufunge Arafa.

Sasa kwa ajili ya kutafautiana kwetu; sisi twaona mwezi kivyetu, na watu wengine wauona mwezi kivyao. Tumekuwa sisi twatatizika, hatujui Arafa ni lini. Sisi kule kwenye Arafa; kunakosimamiwa Arafa. Watu wakismama Arafa, sisi kwetu huwa bado si Arafa.

Kwa hivyo sisi hatufungi siku ile. Twataka kukaa sisi mpaka tutoke dunia hii, tuwe umri wetu sisi hatukufunga Arafa?. Ni hasara ngapi ndugu zangu waislamu?.

Ikiwa sisi tumeletewa zawadi na Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam ; ya kufunga siku inayoitwa Arafa. Na siku hiyo ni ile siku ambayo kwamba waislamu wote husimama uwanja mmoja wakamuomba Mwenyezi Mungu Subhaanahu wa Taala. Na tunatakiwa sisi kwenye miji yetu, siku ile wale wamesimama uwanda mmoja wamuomba Mungu Subhaanahu wa Taala tutangamane nao kwa dua na kwa kufunga.

Lakini sisi huwa siku ile waliosimama wao kule, kwetu si Arafa bado. Kwa hivyo hatuiwahi Arafa. Sisi hufunga siku ambayo kwamba ni Idi. Na siku ile watu wale kule huwa hawakusimama. Twatanganya vipi tena dua na watu wa Arafa? *Mafhuum*?

Kitu cha mwisho kwa upande wa kulazimu:- Sisi twatafuta kutangamana. Na kutangamana tumekupata waziwazi kwenye hadithi nyingi za Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam na Qur'an;

Fungani pamoja na funguani pamoja.Fungani kwa kuuona fungueni kwa kuuona . Kwa nini tena tukupoteze kule kutangamana tunakokutafuta, kwa sababu ya shaka iliyoko katika hadithi ya Kureb?.

Hadithi ambayo tunaweza kuiona ni kama kitandawili. Mwenyewe Ibnu Abbas hakubaini ni hadithi gain ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam . Na ikibaini haiungi mkono upande ule, inaunga mkono upande huu. Tukaacha hadithi zilizo wazi wazi kwa hadithi ambayo kwamba ina matatizo ya kuifasiri. Na hata ikifasirika haiungi mkono hoja hii.

Upande wa kutolazimu:
Wameshikilia mas'ala ya kukhitilafiana matlai. Aliponielekeza sheikh kwenye kwamba ningesoma kipande cha maneno ya upande wa pili. Nawaambia, wameataja pale mbele kile kwenye kipande nilichosoma, ya kwamba, lakini Fulani na Fulani na baadhi ya wanazuoni wa Shaafi–iy, wametaja ya kwamba matlai huzangatiwa .

Lakini huja yangu hapa ni moja mimi; Ni kwamba liko wapi jambo la matlai?. Nani kalitaja? Wapi limetajwa katika hadithi za Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam ?, baasi!. *Hal dhukira haadha, hal- jaa- a dhikru lil matlai fiy ahaadidthi Rasuuli Llaah swalla Llaahu alayhi wassallam?*. Laa ! Kumetajwa matlai, yameelezwa khabari ya matlai? Kuko mahala kwaashiriwa matlai?; Hakuna!.

Kisha msimamo wa wafuasi wa imamu Shaafi.

Tumeeleza ya kwamba watu wa imamu Shaafi wenyewe hawakusimama msimamo mmoja katika hili. Kwa hivyo hata tukitaka kuwafuata nyinyi watu wa Shaafi. Nyinyi wenyewe hamujawafikana. Twaja vipi sisi na nyinyi mwateta?.

Watu wengi munaowasikia ya kwamba wanamfuata imamu shaafi, mimi nawaambia hawawezi kumfuata imamu Shaafi, hawawezi kumfuata imamu shaafi, na wala hawamfuati.

Juzi juzi kulikuwa kuna tatizo la adhana mbili za Ijumaa. Adhana aliyoiweka sayyidna Othman bin Affan; ya pili. *Lamaa kafura N-naas*.

Vijana wa *ahlusunna* ambao wako Nairobi wakaiondosha adhana ya pili, wakasema tungependa kufanya vile tu alivyofanya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam . Hatutaki adhana ya pili.

Watu wetu waliozoea kuteta yakitokea mambo haya wakapiga kelele nyingi.

Nikashikwa mimi barabarani kwa lazima. "Sasa utatueleza mambo haya ni vipi? Mutaona mulivyo na makosa nyinyi"

Kuna nini jamani, hebu taratibuni!. Na hawa wakija huja kwa kasi na aya za *Idhaa laqiitum fiatan, fathbutuu ---- (8: 45)*. --- na MILTANTS na nini-------- hakuna mambo hayo.
Walipokuja kwa kasi na mimi pale nikawaambia; sasa nyinyi mwalipinga hili kwa sababu gain?. "Kwa sababu hili hukhalifu madh-hebi yetu". Nawauliza nyinyi madh-hebi yenu nyinyi, ni madh-hab ya nani?. Wakasema Al- imamu Shaafiy. Kawaambia*; Maadha yaquul Al imaamu shaafiy lima yata a laqu li adhana in*; Imamu Shaafi asema nini kuhusu mambo haya ya adhana mbili.

Ukiangalia **Afiqhu alal madhaahibil Arbaa** utaona ya kuwa imamu Shaafi kapendelea adhana iwe moja. Asema; Mimi imamu Shaafi napenda moja. Sasa wafuasi wa imamu shaafi wateta na imamu Shaafi mwenyewe. Na wao wajidai kwamba sisi hautmuachi imamu Shaafi.

Na mfano mwengine wa mwisho ili nipate kuondoka. Ni kwamba katika huko kufuata imamu Shaafi ni fat'wa zake. Nadhani katika **fiqhu alal madhaahibil Arbaa jz 2**. ipo hapa.

Msimamo wake imamu Shaafi ni adhana ifasiriwe kwa lugha ya pale mahala. Ha! Iwe ni hapa Unguja,; Zanzibar, mukimsikia mtu juu ya sakafu au katika *loud speaker* MUNGU NI MKUBWAA EEH, MUNGU NI MKUBWAA, mutamfanyaje?.

Kwa hivyo imamu Shaafi ataka hivyo adhana tuifasiri. Na hakuna hata mtu mmoja ambaye kwamba atasema; sisi basi adhana tuifasiri.

Ndugu zangu waislamu, niliyokuwanayo ya kuyazungumza ni hayo. Na namalizia kwa kusema. Msimamo tunaoutaka sisi haupo. Sisi twataka *Ikhtilaaful mattali'i.* hatuna cha kututhibitishia ikhtilaaful mattaali'i.

Sisi twataka kuitegemea hadithi ya Ibnu Abbas , hatuwezi kuitegemea leo. Kwa sababu hadithi ya Ibnu Abbas ilihusu miji miwili; Sham na Madina (Syria na Madina). Leo Syria na Madina zafunga pamoja.

Kwa hivyo ikiwa ni kumfuata Ibni Abbas sisi. Ni lazima mambo haya yangethubutu pale yalipoanzia. Na yalianzia Sham na Madina.
Ikiwa Sham na Madina kwenyewe haya hayawi, yaje yawe hapa kwetu na kwenu?.
WASSALAAM ALAYKUM WARAHMATULLAAHI WABARAKAAT-HU.

- Baada ya mzungumzaji aliyetangulia; sheikh Ahmad Muhammad Msallam kuondoka, mwenyekiti alitoa muhtasari wa kilichozungumzwa halafu akamkaribisha mzungumzaji mwenye hoja za msimamo wa kibakwata kuhusu mwezi, ambaye alianza kwa:-

SHEIKH;NURDEEN HUSSEIN SHAADHLY

Assalaam alaykum warahmatullaah; Alhamdu lillaah rabbi L- aalamiin.
Ni furaha kubwa ambayo tuliyoipata kwenye hadhara hii tukufu inayoshughulikia mambo ya mwezi na mengineyo.

Kwa hadithi ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam isemayo *Man Lam yahtam bi amri muslimiin falaisa minhum* Asiyeshughulika na jambo la waislamu si muislam.

Kwa hivyo toka waliohudhuria na sheikh aliyeakileta mada yake hapa. Tumefurahi sana muda alipokuwa anatugawa baada ya kututaka tuwe kitu kimoja aliposema; *Wa a'taswimuu bi habli llaah jamii anh*; kisha akatugawa.

Akatufanya mashaafiy na sisi. Yaani Answaru Sunnah, ndio muradi nadhani wa Sheikh, na ndivyo alivyosema. Kagawa hapa hapa. Baada ya kusema watu wakiwa jambo lao ni moja, anataka kukutawanyeni; Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam asema Faqtuluuh Man ataa ilaykum, wa amrukum jamianh, yuriidu an yufarriqa jaaatakum faqtuluuh. Hadithi ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam .

Kitu ambacho kimetustaajabisha sisi. Tukafanywa mbali na wao wakafanywa mbali, baada ya kututaka tuwe kitu kimoja.

Jengine lililostaajabisha, Sheikh hapa amesema Hablu ni kamba moja ina meno

mawili. Kamba moja ina majiino mawili.Nayo ni Qur'an na Sunnah. Na wote tumefahamu kwamba iwe hivyo Ingawa muheshimiwa rais alitaja vitu vitatu, hakutaja vitu viwili.

Kataja na Ij-ma-a hapo. Na ndiyo t*adwin* ya mambo, yanakwenda kwa Ij-ma-a na Qiyaas. Haikuwa vitu viwili tu, ikatengenezwa mambo kwa mambo mawili.

Na ndio sheikh akasema, baada ya kuwa yeye mwenyewe anatuletea ushahidi wa Qur'an na hadithi, akaleta rundo la vitabu vya ulamaa. Sijui tutafanya nini! – sijui tutakwenda wapi! ---,l tutafahamuje!--- Ndio Qur'an na hadithi vitabu hivi?.

Hapa kuna ***Nailul Awttaar***, na kuna vitabu chungu nzima ambavyo vimewekwa vine au vitano; vya ulamaa. Akataka maneno ya ulamaa yasipate uwanja, naye akaupanua; akauweka uwanja.

Waqt ambapo yeye anasema "sisi hatufuati mwezi wa Saudia".

Sheikh Nurdeena akainua kitabu kidogo alichokuwa nacho na kuwaonesha wanasemina, huku akifafanua. Inastaajabisha sana kwamba kikao cha Saudia kilichokaa, ambacho kinajulikana chini ya Rabitta – *majlisul majma ah fiy tadliil islaamiy* kilichokaa mwaka 1985.

Mkutano huu wameutoa watu wa Makkah Na ikiwa wakuu waliohudhurdia kama vile ibnu Baaz, na wengine kama hao, kama sikosei. Hapa nitampa mwenyekiti asome vizuri qaraara zilizotolewa kuthibitisha kama kuna kila watu na mwezi wao.

Na itakuwa vizuri sana sheikh hapa akiona waliotia sahahi mkutano huo. Atayasoma vizuri majina yao. Namuomba CHAIRMANA atubainie hapa.

Sheikh Nurdeen akiwa amefunua sehemu maalum ya kitabu, akamkabidhi mwenyekiti wa semina. Mwenyekiti akakichukua kile kitabu na kumtaka yeyote kutoka ukumbini aende akakisome. Hatimaye akakubaliwa kwa ridhaa ya sauti kutoka ukumbini asome yule yule aliyeifungua semina kwa kusoma utaratibu mzima wa matukio; ambaye kwa mara nyengine hakutambulishwa. Sheikh akaja mbele na kusoma:-

Alhamduli llaah wahdah waswalaatu wassalaam alaa man laa nabiya baadah .
Sifa nyingi zinamstahikia Mwenyezi Mungu peke yake. Swala na rehema zimwendee yule ambaye hakuna nabii baada yake; yaani Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam; amma baada
Baada ya hayo:
Laqad Dhaka-ra majma-at fiqhil islaami mas alata ikhtilaafil mattaali i fiy binai ru'yat alayhaa; Asema; mkutano mkuu uliowakushanya wanavyuoni wa fiq-hi wa kiislamu, umeyazingatia masuala ya tofauti za machweo ya jua katika suala zima la kujengeka kuonekana kwa mwezi.

Fa raa-a; Mkutano hou ukaona*; Anna-L-islaama banaa*; kwamba uislamu umejengeka *Alaa annahu diinul yusri wa samaa-nh*; kwamba ni dini yenye wepesi na dini yenye kuwepesisha mambo.

Taqbalu hu fittratu qaaima ; Ambayo dini hiyo inakubalika na akili ambayo haijaathirika; yaani maumbile; *Wal uquuli al mustaqiima*; Pamoja na akili zilizosimama sawa sawa;*fiy muwaafaqati L- masaalih;* Akili ambazo zinakubaliana na yale mambo yenye maslahi.

Fa fiy masaalih thabata alaa ithbaa tihaa bi niyyati bashariyya Laa alaa ittimaadihaa alal hisaabi kamaa tash-hadu bihi L– adillatu shar'iyya L – qaattia kamaa dhahaba

ilaa it-tibaari ikhtilaafi L – mattaali i. Limaa fiy dhaalika minal takhfiifi alal mukalaafiina ma-anh kaunihi. Huwa ladhiy yaqtadhiihi N-na dharu swahiih. Famaa yadda –ih L– qaailuuna min ujuudi ij–tihaadi fiy yawmi swaumi wal ifttaari yukhaalifu bimaa jaa-a shar-ahn., waaqianh.

Anasema kwamba, katika mas'ala ya mwezi wako waliokwenda katika kuthibitisha kuonekana kwa mwezi kwa macho. Si kwa kutegemea hesabu kama vile ambavyo zinashuhudia dalili za kisheria; yaani sheria ya kiislamu(Alqaattia).Nadhani wanachuoni nikisema *Daliilul qaattia* nafahamika. Ni dalili ile ambayo haihitaji tena taawili wala tafsiri.

Kama ambavyo wanaozingatia khilaafu ya machweo kutokana na ule wepesi uliopo juu ya wale ambao wamelazimu(Mukala fiina). Kwamba vipi?, Kwamba hayo machweo ndiyo yanayopelekea uwangalifu ulio sahihi katika suala zima la mwezi kama wanavyodai wale wenye kudai hivyo. Kwamba ni wajibu kuungana watu katika suala zima la kuuona mwezi na suala la kufungua.

Yukhalif limaa ja-a shar'an wa aqlan; Kuona kwamba jambo hili linakhitilafiana na sheria na akili iliyo sahihi. Sijui mwenyekiti nafahamika?. Sheikh Nurdeen akajibu; Naam!,msomaji akaendelea.

Ama Shar'an; Ama tukija katika suala la sharia; *Faqad awrada aimmatu L-hadith*;Wameleta au wamepokea maimatu wa hadithi; *Hadithu Kuraib;* Hadithi ya huyu bwana Kuraib.*Wa huwa anna ummal Fadhli binta l- Haaritha*; Kwamba huyu ummal fadhli bint Haarith. Baathahu ila Muawiya bi Sham; Alitolewa huyu kupelekwa kwa Muawiya, kwenda Sham.

Hadithi imetolewa ndugu mwenyekiti, naisoma kama ilivyo.

Qaala; akasema; *Faqadimtu Shaama, faqaadhaitu haajatan*;Kwamba nilikwenda Shaam, na nikatekeleza yale aliyoniagiza.
Fatuhilla alaiyya shahru Ramadhan; Ukanifikia kule mwezi wa Ramadhani; *Wa anaa bi Shaam*; Na min nikiwa niko Shaam. *Fa raa itu L- hilaala laitata Jum'aa,* Nikauona mwezi usiku wa Ijumaa.

Thumma qadimtu L- Madina;Kisha nikarejea Madina; *Fiy aakhir Shahar*; Mwishoni mwa mwezi.*Fasa alaniy Abdallah bin Abbas (r.a);*Akaniuliza Abdallah bin Abbas;*Thumma dhakara L-hilaala*;Kisha akataja habari ya mwezi. *Fa qaala maataa ra aytum L – hilaala*; Akauliza Ibnu Abbas (R.A) wakati gani mumeouna mwezi?; *Fa qultu*; Nikamjibu;*Ra- ainahu Lailata L – Jum'aa* Kwamba tumeuona mwezi usiku wa Ijumaa. *Faqaala anta ra aitahu?;*Jee wewe uliuona*?.Faqultu Naam!;*Nikasema ndio nimeuona.*Wa ra ahu N naas*u ;Na watu pia wameuona.*Waswaamuu,waswaama Muawiya*.Na wamefunga na amefunga vile vile Muawiya.
Fa qaala;Akasema*; Laakinnaaa raainaahu lailata sabt;*Akasema Ibnu Abbas lakini sisi tumeuona usiku wa Jumamosi; *Falaa naazalu naswuumuu*; Basi hatutoacha

kufunga. *Hat-taa nukmila thala thiin*; Mpaka tukamilishe siku thalathini, *Aw naraahu*; Au tuuone *(*huo mwezi).

Faq'ultu. Nikasema hivi kumwambia, Aw-walaa nakhtafiy bi ru'yati Muawiya?. Hatutoshelezeki na kuuona kwake Muawiya ?. Waswiyaamih? Pamoja na kufunga kwake? Fa qaala Laa! Akasema sivyo! Hakadhaa amaranaa Rasuulu Llaah swalla Llaahu alayhi wassallam. Hivi ndivyo alivyotuamuru Mtume swalaa Llah alayhi wassallam.

Waqad tarjama Al-Imaamu Nawawiy Ameitafsiri imamu Nawawi alaa hadhaal - hadiithi. Kuitafsiri hadith hii, fiy sharhiih alaa Muslimi. Ametoa sherh yake imamu Nawawi kwenye Sahih Muslimu kwa kauli yake mlango unaosema **Baabu Bayyaani anna Likulli baladin ru'yatuh.** Mlango unaosema Mabainisho ya kwamba kila nchi una kuona kwake kwa mwezi. Wa annahu; Na kwamba wao, Idhaa raahuL – hilaala. Wanapouona mwezi, Bi baladin;katika mji, Laa yathbutu hukmuhu limaa baiidu an'hu. Kwamba wao wakiuona mwezi haitothibiti hukumu ile kwa wale ambao wako mbali na wao; yaani ile nchi ambayo iko mbali,

Wa-lam yakhruj an haadhaa L – minhaj; Wala hakutoka katika mwendo huo au njia hii, man akhraja haadhaa L- hadith; aliyeitoa hadithi hii;*min Ashaabil kutubi sitat*. Katika wale watu sita wenye vitabu, *Abi Daudi, wa Tirmidhiy, Wa Nnassaiy wa--------*

Alipofika hapo kulikuwa na minon'gono kutoka ukumbini kuashiria jambo. Sheikh Nurdeen akasimamisha msomaji na akarejea kusema sehemu iliyotangulia na kufafanua.

Walam yakhruj an haadhaa minhaj. Naitakidi kwamba imamu Nawawi hakutoka katika mapito haya*, man akhraja haadha L – hadith*;Aliyeitoa hadithi hii*; min as haabi L- kutubi*; Wale watu sita waliopokea, Abi Dawud, wa Tirmidhiy, wa Nasaiy. *Fiy darjat jumlahu…….*

Sheikh Nurdeen, na sauti ukumbini kwa pamoja wakaruhusu msomaji aendelee. *Wa nattaa Al-islaamu, Al-islamu, Alswaumu wal ifttaardi bi ru'yat L- baswriyya duuna ghayya.* Kuwa uislamu umelieleza, umelizungumza, umelitaja suala la swaumu na kula katika kuonekana mwezi kwa jicho, sio kwa njia nyengine.

Limaa jaa hadithu Ibnu Omar; Kutokana na hadithi ya Ibni Omar;*Qaala*; Amesema Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam; *Laa taswuumuu hataa tarauhu L- hilaala*; Musifunge mpaka muuuone mwezi; *Wa Laa tufttiruu hataa tarauhu* ;Wala musifungue mpaka muuone; *Fa in ghumma alaykum;* Kama yatazinga mawingu juu yenu*; Faqdiruu lahu*; Basi ukadirieni; *Rawaahu Bukhariy wa Muslim fiy swahihi himaa*; Hadithi hii imepokelewa na imamu Bukhari na imamu Muslim katika vitabu vyao sahihi.

Fa haadha L- hadiith; Hadithi hii, *Allaqa L- hukmu bi sabab*; Imefungamanisha hukumu pamoja na sababu;*Alladhiy huwa R-ru'yya*; Ambayo sababu hiyo ni huko kuonekana kwa mwezi.

Waqad tu ujadu fiy baladin; Na huenda, ikapatikana katika mji*, Ka Makka wal Madina;* Kama vile Makka na Madina;*Walaa tuujadu fiy baladin aakhar;* Wala usionekane katika mji mwengine; *Faqad yakun zamaanuhaa nahaaran*; Huenda ikawa labda katika mji ule ni mchana, *In – da L – aakhariina*; Huenda ikawa katika mji mwengine ni mchana, si usiku kama vile ilivyo Makka na Madina.

Fa kayfa yuumaruuna bi swiyaam; Sasa vipi wataambiwa kufunga, *Aw L- ifttaar*; Au kufungua!

Waqad karraara al ulamaau minkulli madhaahibi anna L – ikhtilaaful mattaali-i huwa al mu'utabaru in – da kathiiru;Wamekariri maulamaa kutoka kila madhehebu kwamba tofauti za machweo ni jambo lenye kuzingatiwa katika maulamaa wengi.

Faqad rawwaa Ibnu AbdulBarri al Ij-maa;Amepokea bwana Abdul Barri;*Al- laa turaa fiy maa taba–ada minal buldaani;*Kwamba isizingatiwe suala la kuona mwezi katika miji ambayo iko mbali mbali, *Ka Kharsaan minal Andalusi;* Kama huo mji wa Kharsan ulioko Andalusia (Spain).*Aw likulli baladin hukmun yakhusuh*; Au kila mji uwe na hukumu yake peke yake inayowahusu.
Wa kathiirun min kutubi ahli Almadhaahibul arbaa; Na imeelezwa sana katika vitabu vya hawa wenye madh-hebi manne, *Bi dhikri ikhtibaari ikhteiaafil al mataa li'i* ;Kwa kuzingatia kutaja tofauti za machweo, *Bi addilatil qaaima minal sharianh*; Kwa kuzingatia dalili zilizosimama katika sharia.

Watuttaaliuka al kutubi L – fiqhia bimaa yaashfiy alyhaa; Na vile vile katika uangalivu wa vitabu vya fiqhi ambavyo vimeelezwa kwa urefu zaidi kuhusu masuala hayo.

Msomaji akimuashiria sheikh Nurdeen akasema, Naendelea mwenyekiti!.Naye akatoa ruhusa ya kuendelea zaidi na kukisoma kile kitabu.
Wa amma aqlan] Ama kwa akili tu,
Fakhtilaaafil mattaali'i] Tofuatui za machweo. La khtilaafu Li ahadi minal ulamaa] Siyo tofauti ya mmoja kati ya maulamaa katika suala hili. Li annahu minal umuuri L mushaahada] Kwa sababu ni katika jambo lenye kuonekanwa.

Kufikia hapo mkanda wa video uliotumika kunakili mjadala huu ukakatika kwa kuingia kipande kidogo cha qaswida halafu skh akaendelea:-

…….. katika kuonea hukumu nyingi. Alaa dhaalika] Juu ya suala hilo la mwezi.Alla tiy minhaa awqaati swalaat]. Ambayo miongoni mwake kuna nyakati za swala.

Wamurajaatul waaqiya tuttaaliunaa bi anna ikhtilaafil mattaalii minal umuuri waaqi-iyya] Na kwa hivyo tukirejea hasa katika suala zima linalotuka katika masuala haya linatueleza kwamba tofauti ya machweo ni katika mambo yanayotuka(yanyaopatikna),

Wa- alaa dhwauiy dhaalika] Na katika mwanga wa hayo tuliyoyaeleza. Karrara mjlisul majma'al fiqhul islaami] Baraza la mkutano la majma al fiqhul islaami limeamua, limeazimi. Laa haajatan]
Kwamba hakuna haja. Ilaa Da'awati ilaa tawhiidi L- ahila] Kulingania watu katika kuunganisha suala la mwezi. Wal aayaadi] Na sikukuu. Fil a'almil islaami] Katika ulimwengu wa kiislamu.

Li anna tawhiidihaa] Kwa sababu kuunganisha suala hilo. Laa yakfulu L- wahda – tihim] Halitoshelezi katika kuunganisha umoja wao.Kamaa yatahaawamuhu kathiirun minal mustarshiin] Kama wanavyodai wengi katika wale wenye kuzusha fikra hiyo. Litawhiidil ahilla wal a'ayaad] Katika kuunganisha mwezi na sikukuu.

Wa an tutraku kadhiyatu L – ithbaati L- hilaali] Naliwachwe kadhiya ya kuthibiti mwezi.Ilaa dawri iftahi] Katika daril iftaahi; nyumba ya wale wenye …… ya mufti.

Sauti za kutoka ukumbini zikaashiria kuwa tafsiri imekosewa, wakasaidia kwa kusema – MAHAKIMU!.Walqadha – a] Na wale wenye kuhukumu. Fiy duwali islamiya] Katika dola za kiislamu. Li anna dhaalika awlaa wa adnaa] Kwa sababu hilo ni bora zaidi. Bil maslahat L- islamiya] Kuleta maslahi kwa waislamu.Al aamma] Kwa walio wote.

Wa anna naz-jaf tawhiid al umma] Na kwamba jambo linalotosheleza katika kuunganisha umma wa kiislamu. Wa jama-nh] Kalimaa tuhum] Na kuliunganisha neno lao la kiislamu. Huwa ittifaaqihim] Ni kule kukubaliana kwao. Alaa L- a'amaal bi kitaabi LLaah] Kukifanyia kazi kitabu cha Mwenyezi Mungu; yaani kutenda kwa alilioliamrisha Mwenyezi Mungu. Wa Sunnati Rasuulih] Pamoja na hadithi za Mtume wake Swalla Llaahu alaihi wa sallam . Fiy jami-inh shughuylihim] Katika mambo yao yote.

Wallaahu waliyyu tawfiiq, waswalla – llaahu alaa nabiyyina Muhammad, wa aalih waswahabih.

Wamemalizia hapo na kutia sahihi wafuatao:-

(1) Muhammad Ally Al Harkany – Naibu Rais
(2) Abdullah bin Humeil - Rais almajlis almajma'a Alfiqh
(3) AbdulAziz bin Abdillaah bin Baaz - Mjumbe
(4) Musttafa zarqaa - Mjumbe
(5) Muhammed Mahmoud Swawaaf - Mjumbe
(6) Swaleh bin Luqeymy - Mjumbe
(7) Mohammed bin Abdillah bin Sleym - Mjumbe
(8) Mabruuk Al Awaadhy - Mjumbe
(9) Muhammed Shaadhy Almasiy - Mjumbe
(10) Abdulqaduum Al Haashimy - Mjumbe
(11) Muhammed Rushdy - Mjumbe

(12) AbdilHassan Alil hassan Al Nadwy - Mjumbe
(13) Abubakari Mahmoud Julmy - Mjumbe
(14) Thinein Muhammed Makbuul - Mjumbe
(15) Mohammed Qubaan - Mjumbe
(16) Muhammed Sheikh Khuttaab - Mjumbe
(17) Muhammed Swaleh Adeel - Mjumbe

Kabla kumrudishia sheikh Nurdeen ili aendelee na mada yake; msomaji wa azimio aliomba radhi kwa kosa lolote alilofanya katika tafsiri.

Baada ya kusomwa azimio la kikao cha Makka, sheikh Nurdeen Hussein Shadhly akaendelea na mada yake:-

Ni furaha kubwa kuisikia fat'wa iliyotolewa katika mji mtukufu wa Makkat-al Mukarramah; na wakiwa ndani yake wako wakubwa na wazungumzaji wa kutosha, na wanazuoni wa kutosha kama huyu mmoja mnayemjuua Abdula Aziz bin Baaz.

Mkanda ulikatika kidogo, uliporudi……
Na vile vile tunataka kusema tena kwamba, mara nyingi tunapotaja hapa, imamu Nnawawiy ametia kitu katika tarjma yake. Katika sherh ya Muslim kaweka mlango unaobayyin kula mji una kuona kwake kwa mwezi.

Imamu Nawawiy kama tunavyojuwa, yeye alizaliwa mwaka 631, na jina lake kwa ukamilifu ni Yahya bin sharaf bin Muriy bin Hassan bin Hussein bin Muhammad bin Juma Ibnu Huzaam; maarufu Abu Zakaria. Ni mwanachuoni aliyekufa mwaka 676 hijra.

Nataka kueleza tena watu waelewe kwamba qauli ya hisabu iliyotamkwa hapa ni katika maimamu ni mmoja peke yake. Ahmad Ibnu Hambali. Wengi katika ndugu zetu wa kibohora wanafanya hesabu kwa kutegemea kauli yake.

Wallahi nimeona kitu kibaya kwenye hadhara hii ya mwezi. Anatajwa imamu Shaafi hapa kama mtoto mdogo. Na kama ikhtilafu za imamu Shaafi zielezwe mbele yetu hapa.

Sisi tuko chini ya imamu Shaafiy. Na ndio misikiti imejengwa kwa imamu Shaafiy. Na vitabu tunavyotumia ni vya imamu Shaafiy au As-habu Shaafiy. Na hao kina Nawawiy wamekwenda katika mwendo wa imamu Shaafiy (R.A)

Tunarudi katika maudhui ya ikhtilaful mattaali'i. Kitabu kinachosema ikhtilaaful Mataali'i]. Sheikh hapa amesema hakuna maandishi hayo. Na ndio kitabu FIQHU SUNNA ameandika mlango wa ikhtilaaful matali'i, na ndio Shiekh akasema maneno yake yale.
Namuomba mwenyekiti atoe mahala pale.
Kitabu kikachukuliwa kutoka rundo lililokuwepo mezani.

Ingawa ni kitabu kinasaidia katika mengi ya mambo yao, lakini hawana nafasi kubwa katika mambo ya mattlai.

Baada ya kufunuliwa ukurasa husika, mwenyewe Sheikh Nurdeen akasoma:-
Baada ya kueleza hawa kwamba ni Khittaabul aamu Lijamii'il umma, faman ra-ahu minhum fiy ayyi makaani ka –anna dhaalika ru'ya lahum jami-anh]. Lakini mtazame Ikrima, umtazame Qaasim bin Muhammad, umtazame Qayyim wa Ishaaqa wa swahih i-ndal ahnaafi wal mukhtaari anil shaafi- iyya, yu'utabaru Li ahli Kulli balaadi ru'yatahu.
Sauti kutoka ukumbini zikasikika zikishangilia kwa kutoa takbir ALLAAHU AKBAR!
Mwenyekiti akamtaka sheikh Nurdeen angoje kidogo na yeye akasema;
"JAMANI !,SISI, KITI KINASEMA HAKUNA USHABIKI. JAPO KUWA ALLAAHU AKBAR NI JAMBO KUBWA, LAKINI TUNATAKA HADHARA IWE TULI ISIJENYANYUA HAMASA NYENGINE".

SI KWAMBA TUNAMKATAA MUNGU. HAPANA!.TUMEKUJA KWA AJILI YA MUNGU. NA AKIMALIZA SHEIKH,HAKUNA KUCHANGIA. TUNAKWENDA KUSWALI. BISMILLAH. Sheikh Nurdeen akaendelea:-

Na hiyo mukhtaari anil Shaafi –iyya, annahu yuutabaru Li ahli kulli balaadi ru'yatuhu walaa yalzamuhum ru'yat ghairuhum].
Wala haiwalazimu watu wengine kuuona. Maneno haya yamo kwenye kitabu kile kile kilichokuwa kinatoholewa hapa kwa hamasa kubwa. ALLAAHU AKBAR.

Na vile vile kitabu kingine ALFIQH'U – L ISLAAMIYA juzuu ya 2 imetajwa ikhitilaful mattali'i Na akasema hayawi min aqalli 24 farsakh].

Akasema farsakh ni mail 3. Maili 1 = 400 khattua, na khattua 1 = Nyayo 3. na nyayo 2 = I Dhiraa.
Maneno hayo ameyasema Shaafi-iy.

Tafadhali tupe FIQHUL ISLAMIYA juzuuu ya 2, sahifa ya 607 cha Duktur Wahbat.
Katika kutafutwa kitabu hicho, ikachukua muda kuonekana. Watafutaji wakikichanganya na kutafuta Fiqhu alaa Madhaahibil Arbaa. Sheikh Nurdeen akakionesha kilipokuwa, kikaletwa naye akasoma.

Adillatu Shaafi-iy] Asema huyu; dalili walizozitoa Shaafi wamesema ukionekana mwezi bibaladin lazima L – hukmu bibaladil khaaib, Laa L- baaiid bi hasabi ikhtilaafil mataali'i fil attah].

Na ikhtilaaful Mattaali'i hayawi kwa uchache wa farsakh 24. Wametoa dalili. Istidlaali alaa ittibaar ikhtilafil mattaali'i bi sunna walqiyaas wal ma'aqul Sunna].

Wametoa nini?. Hadithi 2, ile ya Kureib nay a 2 ya Ibnu Omar, na zote zimetajwa hapa.

Naam!. Na wametoa kwa wajih zote. Wajih wa qiyaas, pia wamepimia ikhtilafil mataali'i qamar alaa ikhtilaafil mataali'i shams. Al maudh bi ikhtilaafi mawaqiit swalat].

Na vile vile kwa dalili hizi walizozitoa hawa, katika kitabu hiki inatosha kwamba maneno ya ulamaa hawa watukufu ni yenye kutegemewa zaidi kuliko maneno ya wanaokuja kuharibu umoja wa waislamu .

Akiyasema maneno hayo skh Nurdeen huku anakifunga kitabu alichokuwa akikitolea ufafanuzi. Akachukua karatasi yakie nyengine yenye dondoo, akaendelea:.

Na vile vile tufahamu waqit umekwishapita wa ahli tadwiin, umekwisha waqt wa mujtahidiin. Wakati ule ulikuwa ni nini? .Ni qarne imekwishaaanza, qarne ile ya 2 mpaka karne ya 4, imekwisha!.

Miaka mitten na 50 basi!. Hakuna tena haraka za tadwiin zilizozidi lililokuwa wakati ule; Ahli tadwiin. Na ilikuwa ni waqt wa aimal mujtahiidiin.

Wakati ule ndio unaitwa waqt wa tadwiin. Sisi sasa kupokea maneno ya wanazuoni waliyoyasema, maneno ya wanazuoni waliyokata.

Na Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam amesema sanna kukhusu jambo hilo. Na Al ulamaa humu warthatul anbiyaau]. Haiwezi kuwa hata kidogo, kuwa leo imamu Shaafi aseme neno au watu kama hao waseme maneno. Baadae waje watu wengine wayatohoe.

Mpango wa zamani ulikuwa namna gain?. Tashriin fiy haadhal ahad. Ulikuwa Qur'an na Sunna na Ijmaa-nh na Ijtiha-ad na Qiyaas. Aw ya-ati ttariiqu min tturuuqil istinbaatt]. Sio njia ya kusema mbili tu.

Mtu mmoja alikaa akaniambia, sisi tunataka Qur'an tu na hadithi. Nikamuambia, Ndugu yaangu! Mwizi ameiba mara tano, utafanya nini? Akashindwa!.

Mwizi ameiba mara 5 !. Mara ya mwanzo utamkata huku. Mara ya 2 utaondoa huku, mara ya tatu ----------, ukimaliza mara 4, toa katika Qur'an na hadithi, akasema aah! Hapo nimeshindwa. Tafuta!

Mtu mara tano kaiba, mwizi!. Nawe hutaki Ijma-anh, hutaki qiyaas. Basi hiyo itakuwa habari kubwa, ameshindwa.

Na kama itatokea mtu katika mkutano huu. Akatoa faida, itakuwa raha sana. Na watu wanaona raha. Lakini hata kuinua kidole hawezi. Ila atategemea maneno ya ulamaa, baasi.

Na binaadamu yoyote asijaribu kwa yeye kujipa ujuzi zaidi kuliko mwenziwe, aa – h!. Wa fauqa kulli dhiy ilmin Aliim].

Na vile vile kama alivyosema rais wetu hapa. Neno linaweza kuja kwa maana haya, na huyu akalifasiri kwa maana haya, kwa kutolifahamu maana yake. Huyu anaweza kufahamu hivi na huyu anaweza kufahamu hivi. Yametokea kwa watu wengi. Yametokea kwa maswahaba. Yametokea kwa mwenyewe Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam .

Swahaba siku ile, ambaye ni Khalid bin Walid, alipotumwa katika kile kijiji. Alikwenda katika wale. Akawauliza mumesilimu?. Wakasema Laa; swaba – anaa, swaba – anaa. Walisema namna hii. Akawauwa.Na akatoa amri kwa kila sahaba aliyekamata teka amuuwe kwa taratibu zinazohusika. Lakini akina Abdullah Ibnu Omar na wengine hawakuuwa watu wao.

Swalla Llaahu alaihi wa sallam

Wakaenda kwa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam .Akaambiwa wee! Khalid umeuwa waislamu kwa tamko la swaba-anaa. Ilimdhihirikia kuwa; tunarudi kwenye kuabudu nyota. Muradi wa swaba–anaa ni tuko ndani ya dini ya sawa, tumeacha dini za ibada mbaya.

Sayyidna Ali alitolewa na fedha kwenda kuwalipa watu. Tafsiri ya kila kitu inakuja kwa maana yake.

Ukimtazama Sayyidna Omar, amekaa kwenye baraza yake. Imeingia kwenye fikra kweli, anatoa fat'wa; anakuja mwanamke kumwambia; Mume wangu anafunga mchana na usiku kucha kwa ibada. Mara tatu anasema mwanamke. Sayyidan Omar (R.A) hakujuwa, hakujuwa kabisa maana yake.

Mpaka mara ya tatu, Kaab minal Answaar, sahaba mmoja alikuwa pale. Akamwambia; "huyu bwana! Kaja kushtaki. Mumewe anafunga kutwa na anaswali kucha. Kutwa, kucha yumo kwenye ibada tu. Jee yeye hana haki? baina ya mume na mke?"

Allaahu Akbar. Akamwambia basi wewe ni Kadhwahu.

Siyo kila mtu, neno lazima alijue. Ni kwisha kwa kujua mtu mwisho wake kuna ukomo. Kule mbele hawezi kujua. Na hakuna ilmu kubwa kama kusema Laa adry. Imamu wetu Malik (R.A) aliulizwa maswali 40. thelathini na tatu alisema Laa Adriy]. Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam alisema Laa adry nisful ilmi]. Sio kila kitu mtu anajuwa. "Mimi nataka kujuwa tu" Wewe ukaona watu wote wajinga. Wewe ndio mwerevu. Neno lile lile linaweza kusema kweli, huku likambadilikia mtu mwengine.

Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam ilikuwa baadhi ya mambo yanamshinda mpaka uje wahyi. Iliposhuka ile aya *KHUDHIL AF'WA WA'MUR BIL URFI WA A'ARDH ANIL JAAHILLINA.] (7:199).* ***Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili***. Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam maana yake alikuwa hayajui, akamuuliza sayyidna Jibril, naye akasema na mimi sijuwi. Akenda kumuuliza Mwenyezi Mungu. Ndipo akamwambia maana yake kadha.. kadhaa…

Na hivyo hivyo zipo nyingi dalili. Huyu maana yake imekuja hii, na huyu hii. WALLAAHU WALIYYU TAWFIQ].

Tunataka wahdat wa kiislamu katika umoja, bila kuwachanganya watu kwa hadithi za Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam zinazoshangilia umoja, kama mulivyosema hapa; Wa'ata swimuu bihabli Llaah jamianh]– aya.

Kwa hivyo tunahitaji sana katika neno hizi tulizozisema hapa. Iwe umoja wetu umejengwa bila chuki wala hivi. InshaAllahu taala kama kunataka kuwa na hadhara nyengine ya kujadili mambo ya imamu shaafi (R.A) na kutiwa ila mambo yake; kuona kama yeye ni mjinga sana au mwerevu sana, tutafanya hadhara kamili misikitini isiyokuwa na gharama yoyote.

Na watu twaweza kufika misikitini tukatoa habari MADDA!! ya imamu Shaafiy, Naam!. Tuko tayari ittaqaariyu wa imamu Shaafiy.
Akasoma kipande kidogo cha beti za kumsifu imamu Shaafi (R.A) kwa sauti nzuri ya mashairi ya kiarabu; na kumaliza mada yake : ***Yaaa man yuriidu mina taaziu Laa. Ha anta haqan qad arafta ma'am Laa. Fajtam'ana ma'a taaiyiy. Inna L-madhaahiba kullahaa maa qaala L – imaamu Shaafiy.***

Wallaahu warasuuluh a'alam.

Baada ya skh. Nurdeen Hussein Shaadhly kumaliza mada yake, wajumbe wawakaenda kuswali Adhuhuri na kula.

Waliporudi msomaji, akasoma Qur'an. Akafuatia mwenyekiti wa semina aliyetoa muhtasari wa mada ya skh Nurdeen. Alipomaliza akamkaribisha mchangiaji mada wa hoja za kiansaar kuhusu mwandamo wa mwezi.

Mwenyewe alijitambulisha, bila kujitaja jina. Lakini kwa maelezo yake ya huko mbele, inaonesha jina lake naye ni **Ahmad.**

SKH AHMAD

Alijitambulisha kwa kusema kuwa; yeye ni mazaliwa wa kizingitini Lamu, sehemu alipotokea mwenzake Shk Ahmad Muhammad Msallam.

Alisomea Kizingitini – Lamu. Halafu akasomesha madrasa moja Mombasa.Baadae akaenda kusoma nchini Saudi Arabia. Baada ya kujitambulisha hivyo akaanza mchango wake:-

Bismillaahir Rahmaanir Rahiim]. Ama kulingana na mchango wangu, ni kuhusu kuzitanabahisha vifungu ambazo huwenda pengine sheikh alokuja baada ya muhadhiri wa mada, ima alighafilika nazo au pangine hukuzisikia sawa.

Sheikh, kifungu hizi cha mchango wake ilikuwa ni hadithi ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam inayozungumza Man jaakum amrukum jamianh, yuriidu an yufaariqakum faqtuluuh]. Aw kamaa qaala rasuulu swala Llaahu alayhi wasallam.

Maana ya hadithi ni kwamba, yoyote ambaye amekuja, na jambo lenu ni moja, ataka wafarakanisha basi muuweni.

Nafikiri Sheikh kidogo kama lau angefikiri kidogo kisha akajiuliza suala. Mbona tuko hapa?. Nafikiri angepata jawabu.

Sisi hatukuja hapa tukiwa ni wamoja. Ndio maana kukawa husimama fulani akazungumza, kisha akasimama na mwengine.

Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa huko nje sisi tuna tafauati. Huko nje tuna ikhtilafu. Kwa hivyo ikhtilafu ni kitu kiko. Na hakuna yoyote ambaye aweza kuthibitisha kwamba ikhtilafu hatuna.

Na ikiwa aweza kuthibitisha aje tuulizane tena tunkuja hapa kufanya nini?. Kwa hivyo ikhtilafu iko. Hapa tunkuja kutafuta njia sasa ya kuiondosha ikhtilafu. Ndipo tukakutana hapa.

Kadhia ambayo imeanza kuzungumziwa kutoka usubuhi, ni kadhia ya kulazimu watu fulani kufunga kwa kuonekana mwezi shemu fulani.

Wakenya wafunge ikiwa mwezi umeonekana Zanzibar?. Ikiwa mwezi umeonekana Zaire, Mzanzibari afunge?. Ndiyo kadhia iliyokuwa ikizungumziwa.

Kutokana na tatizo hili ukafikilia katika mas'ala ya ikhtilaful mattaali'i, it-tibaaru ikhtilaful mattaali'i na Adamu it-tibaaru ikhtilaful mattaali'i].

Mzungumzaji aliyezungumza alisema hivi:Kadhia ya ittibaari ikhtilaafil mattaali'i katika misingi ya sheria kwenye Qur'an na Sunna Mulghaatu Laa mahaala lahaa minal I-iraabi]. Ndivyo ilivyozungumzwa.

Wanatahadda L – qaailiina bi-ittibaaril ikhtilaafil mataali'i an yaatuu bi hadiithin waahidin swahiih, aw dhaifin aw hata L maudhui].

Walete hadithi moja tu ambayo inswihi kwa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam , kwamba Mtumi aliliweka kwenye akili yake. Aliwafundisha waislamu kwamba ikhtilaaful mattaali'i shaaiun muutabaru fiy Ruudhi LLaah. Twasema hata dhaif au hata maudhui.

Hili ndilo lililozungumzwa. Huwa twangoja jawabu kwa hamu. Lakini sheikh alokuja na mchango baada ya muhadhiri wa mada, bado hakutuonyesha dalili ya kutosha kwamba yatoka kwa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam . Ya kwamba riwaya hii yathibitisha ittibaarul mataali'i. Kisha tutafautiane baina ya kuithibitisha riwaya hiyo au kutoithibisha.

Kwa hivyo mpaka sasa tunalosema ni kwamba, bado hatujapatiwa dalili ya kutuondosha pale tuliposema kwamba hatuwezi kuondoka; kwenye msimamo wa sunna

kwenda mahala pengine popote. Ila tuondoke kwenye msimamo wa sunna twende kwenye sunna. Kwa hivyo hatujaondoshwa. Mpaka sasa. Tukali tunkalia katika kiti cah sunna.

Kisha, Sheikh Muhadhiri akatoa mchango wake katika alilozungumzia. Mimi nimefahamu kitu kimoja, kwamba yeye mwenyewe; sheikh Nurdeen katika mchango wake alikuwa akijimaliza mwenyewe. Qadha alaa nafsih binafsih.

Kwa sababu katuthibitishia, katuelezea asru tadwiin,kwamba asru tadwiin hii kutoka kwa Mtume Swalla Llaahu alaihi wa sallam mpaka kupitia kwa mainamu. Mambo yalikuwa yakizingatiwa hapo. Lakini kisha katuletea qarraraati za majmaul fiqhil islami, uliosimamiwa na Rabittatul Allaamil Islaami uliofanywa Saudia, Jeddah au Makka.

Tukimuuliza bwana aliyetoa mchango Qarraraati hizi ziliandikwa fiy asri tadwiin, fiy asri maa qabla tadwiin, au zilikuwa ni baada ya tadwiin mpaka tuweze kuzitegemea?. Kwa hivyo pia mpaka sasa qarraraati hazijaweza kutufaa kwamba ni dalili.

Pamoja na kwamba lau tutaziangalia qarraraati zilivyo mwanzo, na zilivyo mwisho, hazizungumzii ittibaaru almattaali'i wala adamu itiibaarul mattaali'i.
Lakini qarraraati zinavyozungumzwa, ni kikao kilichokusanyika, chaitaka Rabitta isiiingilie mambo ya mwandamo wa mwezi. Kulazimisha, kumtaka Mzanzibari afunge kwa kufuata mwandamo wa watu wa Kenya. Wala watu wa Kenya kufunga kwa kuonekana mwezi wa Zanzibar. Waambiwa kwamba waachiwe, kila watu wa mahala wajiamulie wenyewe.

Ndipo tukakusanyika hapa, watu wa sehemu za karibu kujiamulia wenyewe, tutafunga vipi? . Haadhaa kullu maa fiy qarraraati].

Kifungu kingine ambacho kilikuwa kina ithara, ambacho si kizuri, cha kuonesha kwamba, Ah! Allaahu akbar]. Sisi sote ni Mashaafi. Lakini hata kama si mashaafi, sisi hatumtaaradhi Imamu Ahmad bin Hambali; ambaye mimi nitasema naye ni Shaafi. Ahmad sikumfuata Ahmad, twaweza kusema hivyo pengine, inswahakum].
Itakuwa vipi sisi kumtaja Imamu Shaafi kama kumtaja mtu mwengine?. Sheikh Nurdeen katika kutuzungumzia sisi, kwamba Shaafi ametajwa kama mtu wa kawaida. Ni maonevu, kutuonea.

Kwa sababu sote tulisikia tukisema kwamba AL IMAAM SHAAFIY. NA HAKUSEMWA VIBAYA !. Liliotajwa ni kwamba Imamu Shaafiy mwenyewe hakuizungumzia mattlai. Kuzingatiwa mattlai au kutozingatiwa.

Mwenye hoja na atuoneshe kwamba Shaafiy, Laa! Kaizungumza kwenye kitabu chake fulani, kuzingatia matlai.

Twendeni kwenye kitabu cha Imamu Shaafiy; UMMU, au pengine kwenye kitabu chake cah RISALA. Tuangalie kaizungumzia matlai?. Kilichozungumzwa ni kwamba, wafuasi wa imamu Shaafiy; baadhi ya wafuasi wa imamu Shaafiy. Laa si imamu mwenyewe.

Na tuliyoyasema au tunayoyasema, kwamba sisi hatumpati Shaafiy, hatumfikilii Shaafiy, bali hatumfuati Shaafiy.

Basi licha ya kumfuata Shaafiy, naweza kusema hata vitabu vya Shaafiy tukivisoma hatuvifahamu kama atakavyo Shaafiy. walimathalu fiy dhaalika].

Nitapiga mfano, wa namna ambavyo sisi hatumfikii Shaafiy, au hatuvifahamu vitabu vya Shaafiy.
Yaa Arbaabal Mattaali'i!. Wale ambao wasema ikhtilaaful Mattaali'i yu-utabaru, turudi tena katika saumu ya Arafa.

Tunavyofahamu kwenye vitabu vyetu; watu wa Shaafiy, ni kwamba Yustahaabu swaumu Arafa yawmu kam?]. Ni suna kufunga Arafa siku ya tarehe ngapi?.
Ukumbi ukajibu, TISA, Sheikh Ahmad akaendelea:-
Twakubaliana tisia?. Haya, vitabu vinavyoelezea ni Sunna kufunga siku ya 9 ya Arafa viliandikwa wapi?. Viliandikwa Kenya? . Nafikiri sote twakubaliana kuwa havikuchapishwa Kenya.

Ikiwa ni Shaafiy. Aasha fiy Masri, wa aasha fiy Baghdaad]. Ikiwa ni Maalik aasha fiy Madina]. Abu Hanifa aliishi upande wa Shaam. Shaafiy hakuishi *EAST AFRICA!*.

Shaafiy aliishi ama Masri au Baghdad. Akisema Shaafiy ni suna kuifunga siku ya tarehe 9, huwa si tarehe 9 ya Kenya wala ya Zanzibar. Huwa ni tarehe 9 ya Misri au Baghdad pale alipoishi yeye.

Na Imamu Ahmad akisema ni suna kuifunga siku ya Arafa akusudia siku ya tarehe tisia ya mahala alipoishi yeye. Hivyo hivyo ndivyo atakavyosema Abu Hanifa, na ndivyo atakavyosema Maalik. Jee tunaosema kwamba ikhtilaaful Mattaali'i muutabaru, siku ya tarehe tisia kwetu ndiyo siku ya tarehe tisia aliyokusudia Imamu Shaafiy?.

Sisi twasema matlai ni tofauti. Shaafiy asema tufunge tarehe tisia. Tarehe ya kwetu si tarehe tisia ya Misri,si tarehe tisia ya Madina kwa Imamu Maalik. Kwa hivyo sisi hatumfuati imamu Shaafiy. Itakuwaje basi kuwa ni mashaafi?.

Kifungu kingine kilichozungumzwa, kwamba mambo yaliyozungumzwa hapa ni mawili. Tumezungumziwa Qur'an, tumezungumziwa hadithi. Hakukuzungumzwa Ijmaa-nh]. Haikuzungumzwa Qiyaas wala hakukuzungumzwa Ijtihadi.

Ijmaa-nh inakuwaje?. Qiyaas kinakuwaje? . Ijtihadi inakuwa vipi?. Tukizungumza Qiyaas twakusudia kiasi gani?. Twakusudia alqiyaas Shaar – iy au twakusudia kiasi chetu cha Kiswahili.

Twakusudia al Qiyaas Shaar–iy. Ikiwa ni hivyo, wanazuoni wa Usulul fiqh watwambia hivi: Ilhaqu far-inh bi asli Li ishtiraqihimaa fiy illati hukmi. Walhukmu yajiibu an yakuuna mansuusan alayhi fil asli]..

Kwa nini tukatumia Qiyaas. Huwa tunakwenda palepale kwenye Alkitaabu wal ssunna. Kwa hivyo kukitajwa Qur'an na sunna kuwa ni vitu viwili, huwa ni jaamiu Shaamil].

Tukisema ijtihaad fiy maa najtahid. Najtahidu fiy nafs. Walaa najtahidu khaarijan Nafsi]. Na tukizungumza Ijtihaad, jee na sisi leo twaweza kuwa na Ijthaad? . Ikiwa hatuwezi ni kitu gani chatunyima?.

Ikiwa twaweza kujitahidi hivi leo, anhaa!. Tuko katika asru tadwiin, au maa baada asru tadwiin].

Hakutuelezea Qiyaas, hakutuelezea ijmaa-nh. Pamoja na kwamba twakubali Al ilmu qaala Llaah, qaala rasuulu Llaah, wal ijmaa-nh wal qiyaas, in swaaha] .Elimu ni Mwenyezi Mungu kasema, Mtume kasema, Ijmaa-nh na Qiyaaas ikiwa zimesihi. Huwa bado hatujajifunga muhanga, kwamba sisi twapingana na Ijmaa-nh. Ijmaa-nh imezungumzwa na Qur'an. Hatuwezi kwenda kinyume na Qur'an

Nukta nyengine ni kwamba, muhadhiri wa mada alileta mlolongo wa vitabu baada ya kutwambia turudi katika Qur'an na hadithi.

Kitabu cha kwanza kilichoashiriwa ni **Nailul Awttaar**. Shawkaniy katika Nailul Awttaar aizungumzia nini? Wasomi wapo hapa.

Said Saabiq katika **Fiqhu Sunnah** aizungumzia nini?. Na vitabu vingine ambavyo ni Kutubul furui, tulivyovileta hapa. Lengo ni kuwathibitishia washiriki, wasomi na wasiokuwa wasomi, namna ya mambo yalivyo tofauti kwa wanazuoni wetu wenyewe kuhusu tatizo la matttlai.

Twaambiwa masafatul qasri] ndiyo ittibaarul matlai]. Wengine wakwambia baina ya mji mmoja ukiweko juu, na mwengine ukiwa chini ndiyo ittibaarul matlai].

Wengine wakwambia amri ikitoka kwa Al amiiri au Al Imaamul Aadham; Al hukmu yaummu Lijaamiiul buldaan].

Lau kama kungekuwa ipo nassi ya kisheria. Lau ingekuwa kuna ijmaa-nh ya wanazuoni, kwa nini ipatikane tofauti hizi, katika kuhadidi masafa ya matlai?

Ni kwamba ni ijtihadu za wanazuoni, wajazaahumu Llaahu khairan alaa ijtihaadihim]. Wa laisa kullu mujtahidin muslim]. Si kwamba kila mtu akifanya ijtihadi huwa amepata.

Mujtahid huwenda akafaulu akapata sawa, falahu ajraan]. Na huwenda akaikosa sawa, falah u ajru Llah.

Kadhia ya Ijtihadi na Al masaailu ijtihadia], si kwamba ni masuala yana undani ambao haueleweki. Wanazuoni wameelezea ikiwa twawaita watu wende kuwafuata wanazuoni, basi tufuate kila linalosemwa na wanazuoni***!. Ijtihadi ya mwanachuoni yoyote si huja kwa ummati Muhammad***.
Mzungumzaji aliyasema maneno hayo kwa Mkazo kabisa, akaendelea:
Ijtihadi ya mwanachuoni ni wajibu wake. ; yeye mwenyewe alofanya ijtihadi atumie ijtihadi yake. Hawezi kunilazimisha mimi!.

Na masuala haya yako wazi wazi kabisa katika vitabu vya usulul fiqh.

Mtu aweza kurudia kitabu chochote cha **usulul fiqh,** asome babul ijtihad. Awaangalie wanazuoni namna wanavyoizungumzia Ijtihadi.

Bila kuchokozwa na mtu yoyote, Sheikh Ahmad akazidi kuzungumza kwa mkazo.

Hakuna mikao katika uislamu. ***Uislamu ni mmoja. qiblatun waahida, ilaahun waahid, diinun waahid, wa hilaalu LlAAH***. Ndio msimamo wa Uislamu.

Wala tusiende kumpapia Shaafi kwa makucha, wala Ahmad, wala Maalik. Wenyewe wakwambia: Laa tuqaalidniy, walaa tuqaalid Maalika] Usinifuate mimi, wala usimfuate Maalik. Kwa nini umfuate kwa lazima wewe! ?, na mwenyewe hataki kufuatwa.

Maalik akwambia kullu waahidin yu ukhadhu min qablihi wa thulatuh]. Hata yeye pia ajitolea ushahidi kuwa langu pia larudiwa. Wewe kwanini ukasema Laa !_ _ _ imetoka wapi?.

Mwisho natija tutakayofikia, tutafika hapa. *Labiya hadith rasuulu swallaLlaahu alayhi wassallam. Amilnaa walaa bil aimati qalladnaa]*..Maneno ya Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam Hatukuwafuata, wala maimamu vilevile hatukuwafuata.

Kwa sababu maimamu wakwambia wenyewe. *Laa tuqalidniy]*. Simkumbuki ni Shaafi au N-nani. Asema; *Laa tuqalidniy walaa tuqalidi Maalika*].Usinifuate mimi wala usimfuate Malik. *Walaakin khudh min haithu akhadhuhum*]. Chukua pale alipokwenda chukua. Huu ndio msimamo wa maimamu.

Wewe usemae kwamba mimi nitajifunga kamba na imamu Malik. Anapoingia imamu Maliki ndipo nitakapoingia mimi. Atakapokaa yeye ndipo _ _ _ . yeye mwenyewe akwambia usinifuate bwanaa!

Watuaswi L– laaha wata'atakid hubahu.

Inna 'L-muhiiba liman yuhibu yasiluhu].

Wamuasi Mungu na il-hali waitakid kuwa wampenda ?. Usijidai kuwa wampenda. Mtu humfata mpenzi wake kwa analo litaka!. Na maimamu wakuwambia jitahidi mwenyewe!.

Aquulu qauli hadhaa, wa astaghfiru Llaah L–adhiim.

Wassalaam alaykum.

SHEIKH BA HASSAN.

Baada ya mchangiaji huyo kuondoka. Mwenyekiti wa semina akatoa muhtasari wa aliyozungumza. Halafu kukawa na mikono mingi iliyonyooshwa kutaka kuchangia majadala wa mwezi. Mwenyekiti, skh Ahmad Zuberi akamchagua Shk Bahassan kwa kusema:
Mikono tunaiona mingi, inayotaka kuchangia. Tunamnyanyua ustadh, Bismillah. Tafadhali.
Ustadh aliyechaguliwa akaanza kwa: **Assalaam alaykum _ _** .Baada ya salamu akasoma dua ya ufunguzi wa maneno atakayoyasema, halafu akajieleza kwa kusema:- Mimi ni sheikh Bahassani. Nimezaliwa Lamu. Nimesoma Riadha, na sasa nasomesha Riadha;Lamu.

Baada ya kujitambulisha hivyo, akasoma aya ya Qur'an, Surat As- Saff (61:8) isemayo:
{ ***WANATAKA KUIZIMA NURU YA MWENYEZI MUNGU YA (UISLAMU) KWA VINYWA VYAO; NA MWENYEZI MUNGU ATAKAMILISHA NURU YAKE IJAPOKUWA MAKAFIRI WATACHUKIA***}
Akasoma tena aya ya Qur'an, surat Al-baqarah (2: 189):-
{***WANAKUULIZA HABARI YA MIEZI, SEMA HIYO NI VIPIMO VYA NYAKATI KWA AJILI YA WATU NA HIJA _ _ _ _*** }

Ndugu zetu, muhadhiri wa kwanza wa mada hii na mshangiriaji wake, wamesisitiza sana kuwa kuzumgumzwe kuhusu Qur'an na hadith. Na mimi pia nikiwa kama ndugu yao, Ansaar Sunnah nitatumia Qur'an na hadithi.

Neno *SHAHIDA* halina maana ya kuhudhuria tu. Kwenye Qur'an imekuja mara nyingi. Sehemu nyengine ni kushuhudia; mfano aya ya 18 ya surat Al – Imran (3:18) :

SHAHIDA ALLAHU _ _ _ شَهِدَ اَللَّهُ أَنَهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ
{***MWENYEZI MUNGU NA MALAIKA NA WENYE ELIMU WAMESHUHUDIA KUWA HAPANA MUNGU ILA YEYE _ _ _ _*** }
Mungu hakuhudhuria, bali aliona. Ikiwa ni kwa macho mawili, matatu.
Mawaqiitu]. Kwenye aya ya (2: 189) si kwa ajili ya masahaba tu. Ingekuwa ni hivyo Mwenyezi Mungu angekuwa na hiyari kuwaambia *MAWAQIITU LAKUM*. Lakini ni kwa ajili ya watu wote, wa zama zote. Ndipo ikaja ***MAWAQIITU LIN – NAAS***.

Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam amesema Ibnu Abbas (R.A) ni *HIBRUL UMMA*. Itakuwa ni kumuangusha Qima tukisema Ibnu Abbas hakuifahamu vizuri hadithi ya Kuraib.

Ibnu Abbas ndiye aliyeifahamu hadithi ya Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam aliyoipokea Abu Huraira isemayo swuumuu liru' yatih wa afttiruu liru' yatih _ _ _]

Hadithi ya Kuraib, ni hadithi sahihi kiabisa, si athar. Kwa sababu Athar ni kitu ambacho kimezungumzwa na sahaba, na hakikupelekwa kwa Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam.

Wenye elimu ya hadithi watwambia, hadithi ikija kwa lafdhi kama *AMARANAA, LUHIINA, UMIRNAA, NAHAANAA* si athari, ni hadithi kama hadithi nyengine.

Ikiwa Ibnu Abbas kaifahamu hivyo aliposema *HA KADHAA AMARANAA RASUULU LLAAH]*, basi hatuna sababu tena ya kuziendea Aqwaali za ulamaau.

Katika Fiqhu Sunnah uk. wa 436 chapa ya Beirut, Said Saabiq asema mattlai ndicho kitu chenye kuonekanwa na chenda kulingana na ulimwengu.
Ikiwa imethubutu *MAWAQIITU LIN – NAASI WAL HAJJ]*.Tujuwe kuwa hija ni ile ile moja, lakini mawaqiitu ni Ahilla. Na Mwenyezi Mungu Kaiweka dhwamir ya Hiya kurudi kwa Ahilla, kuonesha kuwa dhwamir ya muanathu yarudi kwa jam'u.

Qur'an kwa lafdhi hiyo yatufundisha tusome elimu ya miiqaatu. Si lazima inenwe wazi. Mfano Mwenyezi Mungu aliposema katika Qur'an (67:15) _ _ _ *FA- MSHUU FIY MANAAKIBIHAA]*. { ***YEYE NDIYE ALIYEIFANYA ARDHI IWE INAWEZA KUTUMIKA KWA AJILI YENU. BASI NENDENI KATIKA PANDE ZAKE ZOTE NA KULENI KATIKA RIZIKI ZAKE. NA KWAKE YEYE NDIYO MAREJEO.}***

Kwa aya hiyo tunaelewa kuwa kufanya kazi ni lazima. Mfano mwengine katika Qur'an (36:69):*WA MAA ALAMNAAHU S-SHIIRA* _ _]. {***WALA HATUKUMFUNDISHA (MUHAMMAD) MASHAIRI' WALA HAYATAKIKANI KWAKE HAYO. HAUKUWA HUU ILA NI UKUMBUSHO NA QUR'AN INAYOBAINISHA}***

Wanazuoni wakaona SHI'IR (mashairi) ni elimu ya kusomwa. Ikiwa twajadili mada ya mwezi, ni lazima tujihakikishie elimu ya *miiqatu*, tunaielewa.

Ndipo wanazuoni wa *miiqaat* wakaweka vitu wanavyoviita *TTUUL, KHAATTUL ISTIWAAU* na kadhalika. Daraja moja ni dakika 4.
Ikiwa hadithi ya Kureib itakuwa bado twaitilia shaka basi itakuwa hakuna kitu kingine kinachofaa. Ni kama kulazimisha mchana utolewe dalili kuwa ni mchana.

Wanazuoni 17 waliokubali katika qaraari mujtamaal fiqh, hawakujitahidi na sisi pia hatujitahidi. Ni kwamba walishazungumza na kufikia azimio kuwa kila watu na matlai yao.

Jee, itafikia pahali, mwezi ukionekana Zanzibar maeneo mengine yakubali kupokea mwezi wa Zanzibar?. Au ni sisi Zanzibar tu, tupokee miezi yao?. Ati kwa kuwa sisi twataka uislamu twataka umoja!. *Laa nuuminu bi baadh wa nakfur bi baadh].*

Ni sharti ije ifike kila pale ambapo Ansaar Sunnah wataka tuchukue mwezi wao, na wao wachukue mwezi wetu. Jee ni *maaqul* hiyo?.

Asemaye kuwa Ibnu Baaz aliirudi kauli ya kikao kile cha wanazuoni 17, basi atuhudhurishie kitabu kinachosema hivyo.

Hadithi iliyokuja; *yawmu taswuumuuhu wa yawmu tafttiruun, wa yawmu tad'ha huun].Yawmun,* ni kuwa kuna siku fulani. Nataraji muhadhiri wa mada kama hii hana upungufu wa kuelewa lugha ya kiarabu, na kwamba yawmun ni *naakira*, na ni siku yoyote.

Kama ingekuwa imekuja kwa *maarifa* ingekuwa ni siku maalum. Watu wote siku hiyo wafunge, watu wote wale au watu wote wachinje. Lakini *yawmun* ni siku yoyote kulingana na mattlai yenu, na wengine kulingana na mattlai yao.

Kwa hivyo hakuna dharura ya kuwa ni lazima mwezi ukionekana miji fulani iwe na sisi sote tufuate miji kama hiyo.

Hii ni kwa sababu ya Qur'an na hadithi, hatukutoka!. Tunazo qauli kadha wa kadhaa za aimma wote wanne, kila aimma azungumza yeye na as –habi zake kuhusu mas'ala ya matlai.
Hizi ndizo hoja zetu. Nataraji nimeeleweka vyema. Wassalaam alaykum.

- HOJA ZA KIBAKWATA
- **SKH AHMED KHATIB WA MOMBASA**

Mhadhir aliyepata nafasi baada ya Skh Bahasani ni skh Ahmed Khatib.
Katika kujitambulisha, alisema yeye ni mkenya. Amesomea Kenya na kwahala kwengineko, moja wapo ni Zanzibar.
Kabla kuendelea. Alitaka aletewe chaki na ubao wa kuandikia. Mwenyekiti wa semina akapendezewa na wazo hilo, na akataka mzungumzaji asiendelee na chochote mpaka vifaa hivyo viletwe.
Skh Ahmed Zubeir, akasema, yeye alijua mapema, mambo haya ni makubwa hivyo alitaraji vifaa hivyo vingetayarishwa mapema.
Kwa vile vilikuwa viko mbali, skh Ahmed Khatib ikabidi aendelee na mchango wake.

Akasema. " ingekuwa ni vyema kila pote lingekuwepo hapa, ili liweze kutoa *contribution* yake.

Bil itiraf]; ni lazima tuseme skh Ahmed Al-khalily; mufti wa Oman, ana muhadhara mzuri kuhusiana na mas'ala haya. Amezunguka kwenye madhehebu mbalimbali ya kiislamu. Kwa sababu hili tatizo si la leo wala la jana. Lipo tangu zamani.
Tatizo kubwa limezungumzwa na muhadhiri alonitangulia kuhusu tafsir ya aya ya (2:189) iliyotaja neno mawaqiit. Lakini imetupa wazo zuri zaidi.
Qauli isemayo ikhtilaafu ulaamaau Rahma] ni sawa ila *mafhuum* yake ndiyo imekuwa *khattaau*] imefahamika vibaya.
Imamu Jaafar Sadik katika kuitafsiri hadithi hiyo amesema *ikhtilaafu* inayo kusudiwa ni *ikhtlaafu ilaa_ _ _* , yaani kwenda kuifuata elimu kwa yule na yule. Siyo kuhitilafiana kwa kutokuelewana.
Qur'aan imeteremka kwa lugha ya kiarabu, hivyo inakubali tafsiri kwa istilahi za kiarabu. Muhadhiri wa mwanzo alisema neno *Shahida* lina maana ya *hudhuuri*, wa pili akasema ni *alima*> kujua, kuelewa n.k. ndivyo Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam akasema *Swuumuu Liru'aytih wa afttiruu Liru'yatih]*.

Inaposemwa *Ru'ya*, hili ni tatizo jengine la kielimu, na ni tatizo la *Ru'yatul hilaal*.
Ikiwa ni hivyo, basi kutakuwa na kanuni za kifizikia juu ya kuona. Kutakuwa na kanuni za kijiografia. Vilevile kutakuwa na kanuni za kihesabu Hasa hesabu ***muthalathatu>*** *TRIGONOMETRY.*
Alipofika hapo vifaa alivyoagiza aletewe vilikuwa tayari vimeshaletwa. Akainuka kuelekea ubaoni na chaki mkononi.
Akaeleza kanuni ya kifizikia juuya mwendo wa mwangaza mpaka unavyoifikia mboni ya jicho. Akachora maumbo mawili ya pembe tatu ya aliyounga sehemu ya ncha moja moja. Mbele yake akachora mboni ya jicho.

Pembetatu mbili akazipa majina ya a,b,c na a,d,e. zote zikaungana ncha ya a.



Baada ya hapo akachora maduara ya njia za sayari angani peke yake, na akachora dunia pembeni,peke yake, iliyoegama kwenye mhimili wake.



✖

s b

Skh Ahmed akatoa majina ya sehemu mbele, juu ya dunia, moja ncha ya kaskazini na nyengine ncha ya kusini ya dunia. Akaelezea jinsi gani sehemu hizo, moja inavyokuwa na mchana mkubwa miezi kadhaa na nyengine usiku mkubwa kwa kipindi hicho. Pembetatu mbili alizozichora, hakuzitolea ufafanuzi wa kutosha. Mimi nilifahamu pembetatu (**triangle**) a,d,e iliwakilisha njia ya mwangaza wa jua, unaotua kwenye sayari yoyote **a.** Pembe tatu abc iliwakilsha njia ya mwangaza kutoka sayari mpaka kwenye mboni ya jicho.

Akasisitiza kuwa kanuni ya kifizikia juu ya mwendo wa mwangaza hairuhusu mwangaza kutoka mwezini, kuonekanwa na kila mtu duniani kwa wakati mmoja. Hii ni kutokana na kuwa kila mtu anakuwa sehemu tofauti ya kijiografia.

Katika ufafanuzi wake wa ziada uliopewa nguvu na muhtasari wa mwenyekiti, alioutoa mwishoni. Ilioneshwa suala la matlai lipo, na kila watu wafunge kulingana na matlai yao.

Akaendeleza mada ya mchango wake kwa kusema; Huu mwezi, hili jua, hii ardhi, vyote hivi ni *makhluqaati Llaah]*. Hatuna shaka nazo.

Mwenyezimungu asema vyote vyaenda kwa hisabu kama anavyosema katika Qur'an surat Alfurqaan, aya ya (25:2) { *AMBAYE NI WAKE UFALME WA MBINGU NA ARDHI WALA HAKUWA NA MWANA WALA HAKUWA NA MSHIRIKA KATIKA UFALME NA AKAUMBA KILA KITU NA AKAKIKADIRIA KWA KIPIMO}.*
Tukiichukua aya hii tukufu tukitia mwezi, jua na sayari tutapata tatizo lililozungumzwa leo la *Miiqaat*. Mtu yoyote akiharakisha bongo yake aweza kuyafahamu mambo haya. Ni mas'ala ya kielimu, na Qur'aan haipingi kuwa sisi tusisome hivi. Ilipokuja katika Qur'an (25:2) *WA KHALAAQA KULLA SHA'IY FAQADARAHU TAQDIIRAN*. ***Qadar*** ni ***Hisaab***. Sasa sisi tunapolazimisha, itakuwa tunafanya ***Ij-halaf***.

Mwenyezi Mungu asema katika Qur'aan (2:185) *: MWENYEZI MUNGU ANAKUTAKIENI YALIYO MEPESI WALA HAKUTAKIENI YALIYO MAZITO.*
Hii *Yuriidu Llaahu Bikum Alyusra]*; katika hali hiyo itakuwa iko wapi?.
Watu watakaokuwa *khatti* ya 180 na walioko 0^{0} greenwhich. Wa huku hawatauona mwezi, na watakuwa wana siku watakula Ramadhani. Sasa itakuwa wanakosa gani hawa? . Kwa sababu hawakuuona, kula Ramadhani ni *jarima.*Ni lazima mambo haya yachunguzwe, ili kila mtu pale alipo asipate jarima ya kumuumiza kwenye moyo kuwa amekula siku ya Idi, au amekula Ramadhani. Mambo ambayo yote mawili ni haramu.

Enzi hizi tulizonazo hakuna mufasir wala hakuna muhadith.Tunachofanya ni kueleza tu mufasir fulani au muhadith fulani alisema nini.Wanazuoni wa fani hizo wapo.
Sisi twazungumza upande wa sayansi. Qur'an na hadithi zatulazimisha tupeleleze zitu kama hizi.Katika Qur'an aya nyengine ya Surat Ibrahim ya (14:33) yatwambia: {*NA AKALIFANYA JUA NA MWEZI KWA MANUFAA YENU DAIMA DAWAMU. NA AKAUFANYA USIKU NA MCHANA KWA MANUFAA YENU}*.

Ili kufafanua hadithi ya Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam yenye kutaja swaumu kum] na yawmu taswuumuhum] skh Ahmed Khatib akatoa beti za kinahau kuonesha neno yawmu ni Naakira na wala si maarifa. Ni siku yoyote, si siku maalum.

Wahadhiri walionitangulia wamekanusha kwamba katika Qur'an kuna *mattlai Qamar.* Wenzetu wamesema kuna matlai shamsi tu.

Matlai Shamsi ipo kwenye aya ya 86 ya Surat Kahf (18:86) isemayo: {*HATA ALIPOFIKA MACHWEA JUA ALILIONA LINATUA KATIKA CHEMCHEM YENYE MATOPE MEUSI*_ _ _ _ }

Tunapata mattlai shams kwenye Surat Qadr (97:5): { *AMANI USIKU HUO MPAKA MAPAMBAZUKO YA ALFAJIRI}.*

Katika Qur'an ni sahiih hakuna matlai Qamar. Lakini tukikubali hivyo basi tukubali kuwa katika Qur'an hakuna ***majaaz*** pia.

Wassalaam alaykum.

- HOJA ZA ANSAAR SUNNA
- **SKH MUHSIN**-MWANAFUNZI WA SKH. NASSOR BACHOO

Baada ya Skh Ahmned Khatib kuondoka, mwenyekiti akatoa muhtasar. Hamasa ya kuchangia ikaongezeka kwa mikono kuwa mingi zaidi kutoka kila upande.

Mwenyekiti, Skh Ahmad Zubeir akamchangua upande wa Ansaar Sunna. Aliyechaguliwa ni kijana aliyeanza kwa kusema:

Bismillaah. Kwa vile muda ni mdogo. Nitazungumza kwa haraka haraka.
Kutokana na haraka hiyo, hakujitambulisha. Lakini kwa lafdhi ya mazungumzo yake, nimemtambua ni mzaliwa wa kisiwa cha Unguja, na kwa marejeo yake ni mmoja kati ya wanafunzi wa Skh Nassor Bachoo. Akaendelea:-

Kwanza narejea kuwa twaweza kuendelea na ikhtilaafu zetu kutokana na hadithi isemayo ***IKHTILAAFU UMMATIY RAHMA***.
Hadithi hii ni dhaifu na imetajwa kwenye vitabu. Tunamnukuu Skh Muhammad Nasrudin Albaniy, asema: *Anna L- hadiithu Laa yaswihu Bal huwa baattilu]*. Asema skh Albaniy; *Qaala AlAllama Subkiy, Lam attifu Lahu alaa sanad sahiih, walaa dhaiifu walaa maudhuui].*

Subkiy asema sijaona sanad ya hadith hii, yoyote. Iwe ni sahihi, dhaifu au hata maudhui. Hivyo hayo si maneno ya Mtume kabisa.Anayekuja yoyote, aseme tu ni maneno yake. Hadithi hii iko kundi moja na ile isemayo*;IKHTILAAFU ASHAABIY LAKUM RAHMA].* Anayetaka marejeo aangalie ***Swifaatu swalatin Nnabiy***.

Tukiendelea kwa upande wa aya zilizotolewa na ndugu zetu waliotangulia.Kuhusu aya ya *Ahilla;* (2:189). Ama aya hii tafsiri yake katika vitabu vyote vya tafsiri iko wazi kabisa, kuwa ni pale makuraishi walipomuuliza Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam*; maa baalul Ahilla?].*Vipi hii miezi?. Mara mkubwa, mara mdogo mara mkamilifu, mara umepungua. Hebu tufahamishe !. Ndipo ikaja ile *jam'u ya Ahilla]*.

Mwenyezi Mungu ndipo akamwambia Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam {*WANAKUULIZA JUU YA MIEZI. SEMA: HIYO NI VIPIMO VYA NYAKATI KWA AJILI (YA MAMBO) YA WATU NA YA HIJA (ZAO)}* -(Qur 2:189)
Ama ikiwa mtu anataka kutumia *Ahilla* kwa sababu kaona jam'u> wingi wa Hilaal ili atie fikra yake, si kwa kurejea *asbaabun Nuzuul* ya aya. Tungemuomba atupe tafsiri moja tu au mwanazuoni mmoja; mufassir aliyetafsir kuwa Ahilla kuwa ni *mattlai L- qamar*.

Halafu *mawaqiitu Lin-Naas* haihusiani kabisa na matlai. Mtume swallaLlaahu alayhi wassallam alivyokusudia na na wafassiriina walivyosema, ni nyakati za watu, kwa namna gani?. Ni kwamba leo unajulikana mwezi umeingia gizani; ni kuvua vibua. Leo umetoka nje, hakuna vibua.

Kwa hivyo, vile jinsi mwezi unavyobadilika ndivyo watu wanavyofanya amali zao katika mwezi.

Halkadhaalika ukimalizika mwezi mmoja unaingia mwengine mpaka mwezi wa Hija.

Kwa hivyo *matlai lqamar* hakuna katika Qur'an. Jambo la kufurahisha ni kwamba Alhabiib skh Ahmed Khatib amekubali kuwa katika Qur'an hakuna *matlail–qamar*, lakini kaenda kwenye hoja za kisayansi.Kuhusu sayansi si suala la mushkel na muda ukiruhusu tutaeleza kwa urefu.
Fat'wa ya Ibnu Baaz imeelezwa kuwa ni hoja kwa vile yeye ni mufti katika Saudi Arabia. Na vilevile wanazuoni wengine ambao ni makadhi na mamufti katika nchi zao.Suala linakuja hapa. Je hoja yake imechukuliwa kwa vile yeye ni mufti na wale wenzake. Ikiwa ni hivyo ,Ibnu Baaz huyu huyu, twaweza kutoa karatasi ambazo zimeenea zinazosema Maulidi hayafai. Jee twamfuata Ibnu Baaz kwa kusema Maulidi hayafai?

Sasa, je tunafuata alichosema Ibnu Baaz au ni kila alichosema kuwa ni sahihi?. Ikiwa ni kwa usahihi wa alichosema sio Ibnu Baaz mwenyewe, basi turudi palepale kuwa;twaweza kurudia na kuhakiki *qarraraa*ti na na maazimio yaliyopatikana, na kusema kuwa hakuna hoja ndani yake.

Kuhusiana na mikutano,huo ni mmoja tu. Mimi naweza kutoa mikutano zaidi ya mitano ambayo imekaa na kusema kuwa mwezi ukionekana sehemu moja, waislamu wa ulimwengu mzima wafuate.

Mwaka 1972 ulifanyika mkutano Misri, na kumetolewa kitabu **ALBUHUUTH**. Kwa bahati mbaya hapa hakuna,lakini namfahamu sheikh ambaye anacho.Sheikh Omar Juma Mayunga, maarufu;anacho kitabu hicho na itifaki ipo kuwa mwezi ukionekana sehemu moja waislamu wa ulimwengu mzima wafuate.

Mwaka 1973 vile vile kulifanyika mkutano katika nchi ya Kuwait. Vitabu vipo, kwa bahati mbaya hatukuvichukuwa hapa; kwa sababu hatukutarajia kuwa vitu kama hivi vya mikutano watu watavifanya kuwa ni hoja.Lakini tunaweza kuvipata ikiwa muda utatosha.

Alipofika hapo akaja mmoja kati ya wasimamizi wa semina kutoka meza kuu na kuwacha kikaratasi kwenye meza mbele ya mchangiaji mada.Aliyewacha kikaratasi kabla kuondoka akaongeza kunong'ona na mtoa mada. Sauti ya mtoa mada ikasikika; Dakika 10 tena!.*Halafu akaugeukia ukumbi na kulalamika kwa hadhara*; Naambiwa hapa, muda umekwisha. *Ukumbi ukatoa sauti ya mshangao*; Aaah! *na sauti nyengine za mchanganyiko wa minong'ono.*

Mtoa mada akaendelea kulalamika kwa uwazi; Haya makubaliano ya dakika 10 yamekuja baada ya mimi kuwa nimeshaomba. Ilikuwa ni haki yangu niendelee kuzungumza nimalize halafu ndipo ije sheria hiyo ya dakika 10.

Ghasia ukumbini zikaongezeka Skh Ameir Tajo akaingilia kati kutaka kutuliza majibizano. Halafu mwenyekit, Skh Ahmed Zubeir akatoa maelezo kwa ukali kidogo;

Maoni hayo ni kabla ya watu hawajatoka nje. Walipotoka nje hoja hiyo imebatilika.

Mtoa mada akaonekana kunung'unika lakini alichosema kutokana na mchanganyiko wa sauti hakikusikika. Mwenyekiti akamjibu:Mimi nina kura ya veto eti!.Unayo habari hiyo?. Mtoa mada akajibu bila kusikika. Mwenyekiti akasema; Basi pata habari hiyo. Mimi lazima nichunge, kwa sababu nikikuacha utakavyo wewe, unaweza ukaenda mpaka asubuhi.
Mtoa mada akaacha kubishana na mwenyekiti na akaomba apatiwe nusu saa. Mwenyekiti akajibu; Usiombe nusu saa, kwa sababu ni lazima akubali mzungumzaji wa upande huu, akupe dakika zake 10. Akaiuliza hadhara; Mnakubali,hamkubali?. Sauti nyingi zikasikika zikijibu; Tunakubali!. Mwenyekiti akamuelekea mtoa mada na kumwambia, Haya Bismillaah.

Kabla hajaanza kuzungumza sauti chache nzito zikasikika; Hatukubalii!. Mmoja kati yao, akaweka bayana pingamizi lao; Huyo msemaji wa huku ikifika muda wake atasema nini ikiwa dakika zake atachukua yeye?.

Mwenyekiti akawajibu; Sio ombi lenu bwana!. Naye mchangiaji akiwa ameduwaa na kukwama kuendelea, akasema tena, sasa akijibizana na wale waliokataa; Mbona wakati ule, ombi la upande mmoja lilipoletwa, sisi tulinyamaza kimya?.

Mwenyekiti akajibu tena; Sikiliza bwana!, Wakati ule hatukuhadidi muda kwa mtu yoyote. Ni kwa sababu maalum. Na bila shaka kila muhadhiri aliweza kueleza kwa upana na marefu. Lakini sasa waqti uko mbele yetu. Na bila shaka kuna wahadhiri tayari wamejitayarisha kwa ajili ya magharib.

Marehemu Skh Ameir Tajo akataka kukatisha mabishano yasiyokwisha kwa kusema ambaye angehitaji wakati wa ziada ingebidi asubiri kesho yake asubuhi. Akatanabahisha kwa kusema; Twataka kuswali sisii!.

Baada ya mashauriano baina ya sheikh Ameir Tajo na mwenyekiti likatolewa tangazo la ufumbuzi wa matumizi ya muda kwa mwenyekiti kutangaza; Tumeamua huyu bwana amalizie dakika za mwenzake aliyetangulia. Na kama kuna hoja zaidi itakuwa ni kesho tena.

Mzungumzaji aliyekuwa akisubiri akaendelea na hoja zake zilizozidi dakika 10 na bila kuendeleza majina ya mikutano mitatu iliyobaki iliyosema mwezi ukionekana sehemu yoyote, waislamu ulimwengu mzima wafuate.Akaendela:-

Na kuhusu kisa cha Kuraib. Kuna watu wanakichukulia kuwa ni hoja pamoja na *ikhtilaaaful mattaali'i*. Pengine pamoja na kauli za baadhi ya watu wa Shaafi.

Kisa cha Kuraib kiko wazi, kwamba haikuwa ni hoja. Kwa sababu tumeona kuwa Ibnu Abbas asema: *Lakinna ra a-inhu lailata Sabt, falaa nazaalu naswuumu hataa mukmila thalathiin aw naraahu]*.

Hii anayosema Ibnu Abbas ni kuonesha kuwa yeye ameuona Jumamosi na watu wa Shaam wameuona Ijumaa. Haina maana kuwa, kwa sababu yeye kauona Jumamosi ndipo afuate watu wa kule kwa sababu ya matlai.

Ninachotaka kuuliza hapa, ni jee haitokei sisi hapa ikawa mwezi hatujauona, na ukaonekana na watu wa bara. Au ukaonekana Unguja tu Pemba usionekane?

Jee ikitokea hivyo ni *ikhtilaaful mattaali'i* nayo?. Ikiwa hoja ni kutokea mmoja akauona na mwengine asiuone, kwa nini tusichukulie kuwa hii ni dharura ilitokea mara moja. Na vipi imefanywa ni hoja ya kufuatiliwa?.

Kitaalamu inajulikana kuwa baina ya Sham na Madina tofauti yao ni 4^{o} longitude na 10^{o} Latitude. Hii kitaalamu si tofauti ya kuleta ikhtilaaful mattaali'i.
Kwa taarifa zaidi. Hivi sasa Sham na Madina hawafungi kwa kukhitilafiana. Ikiwa ni hivyo ina maana kuwa kuuona mwezi Sham na Madina kwa siku moja ni kitu kilichowezekana.

Kwa hivyo kwamba Madina waliuona mwezi siku nyengine si hoja. Hiyo pengine ilitokea tu kwa vile Kuraib alichelewa kufika pale. Na habari hazikuweza kuwafikia watu wa Madina mapema wakaweza kupewa habari za kufunga. Tatizo ni hilo tu.

Jambo jengine, ni kuwa kisa hiki cha Kuraib hatuwezi kukisia na kufanya Qiyaas. Kwa sababu misingi ya Qiyaas inajulikana.Ni lazima pawepo na *Asli*, pawepo na Hukmu, pawepo na Illa na pawepo na Alfardhu.

Sasa hapa; illa Ibnu Abbas hakuitaja kwa waadhihu; kwa sarakha. Kwamba ila ya watu wa Madina kutokuwafuata watu wa Sham ni ipi hasa.Ikiwa ni kutofautiana siku, tumeshasema hata hapa sisi wenyewe tunatofautiana siku kuuona. Sababu hajairejesha ni wapi?. Alisema tu *Hakadhaa amaraana Rasuulu LLaah*].Hivyo illa haiko waadhih.

Illa ikiwa haipo masharti ya qiyaas hayatimii, na hivyo hatuwezi kuifanya hii ni Qiyaas ya kuwa sisi hatuwezi kufuata nchi nyengine unapoonekana mwezi.

Laa tukichukulia kuwa illa ipo na hii ni Qiyas. Tuseme tunaweza kuchukulia ***Assumption*** hiyo, na sababu ya mattaalii'i.Lakini ikiwa utawafuata watu wa *metrology,* Sham na Madina masafa yake ni wastani wa meli 700.

Ikiwa tutafanya hicho kuwa ni Qiyaas basi ina maana kuwa kuanzia meli 700 ndipo watu wasifuate nchi au sehemu nyengine. Chini ya hapo haitokuwa ni Qiyaas.Sasa jee katika kitabu cha Hidayatul Atfal uk. 53, inaposemwa ni lazima tuhitilafiane kuona mwezi kwa masafa ya meli 560. Ikiwa marejeo ni kisa hiki,hizi meli 560 zimetoka wapi?.

Au kama ilivyoelezwa katika kitabu cha **Fiqhu Alal Madhaahibil Arbaa** kuwa ni farsakh 24.

Farsakh imetofautiana katika makamusi. Ama ni meli 3 au 5.Ukizidisha mara 24 utapata meli mpaka 120.Ikiwa ni mattaali'i ya meli 120, mbona hatukufuata kama ilivyo kwenye kisa cha Kuraib ambapo ni meli 700?.
Sisi ketu ilikuwa tuanze na meli 700 ndipo tuhitilafiane, lakini sivyo ilivyo. Tutakuta kuwa bado kukitumia kisa hiki, kwamba sisi tunaweza kuhitilafiana haijakuwa ni hoja.

Halafu kuhusu kauli ya swahaba. Kwa watu wa *Usuuli,* kauli ya swahaba siyo hoja. *Al usuliyyuun* wameafikiana kuwa kauli ya swahaba haiwi hoja ikiwa ipo aya na hadithi iliyokuja kwa *swaraakh*.

Tunashuhudia kuwa siku moja Sayyidna Omar (r.a) alikuwa akihutubu,akataka kuweka mpaka wa mahari. Akanyanyuka mwanamke akamwambia "*kaifa taquul yaa Omar*", *Wa llaahu yaquul*:
{NA KAMA MKITAKA KUBADILISHA MKE MAHALI PA MKE (MWENGINE) NA HALI MMOJA WAO (UNAYEMWACHA) MUMEMPA MRUNDI WA MALI. BASI MSICHUKUE KITU CHOCHOTE. JEE MTACHUKUA KWA KUSINGIZIA NA (HIYO NI) DHAMBI ILIYO WAZI KABISA}. **Quraan, Annisaa aya ya 20**.

Hapa Sayyidna Omar (R.A) aliposomewa na mwanamke aya hiyo, kwamba kwanini waweka mpaka wa mahari wewe, na Mwenyezi Mungu kasema hivi. Omar (R.A) akanyamaza halafu akasema; *Aswaabat m'raat wa akh-ta'a Omar]*. Omar (R.A) akakubali kuwa amekosea na yule mwanamke amepatia.

Halkadhaalika tunajua kuwa kitu kikiingia najisi ni majosho saba, mojawapo likiwa ni kwa mchanga. Abu Hurayra anatumia majosho matatu tu. Lakini sisi twafuata saba. Kwanini tusimfuate Abu Hurayra?.Ina maana sisi penye *swariikh* ya aya na hadithi hatuendi kwa swahaba. Tunarejea aya na hadithi siyo kufuata kauli za maswahaba.

Imamu Shaafiy aliulizwa, kama ilivyo kwenye kauli yake ya 1807 ya kitabu chake cha **Al-Risaala**. Aliulizwa ni vipi kuhusu kauli za maswahaba. Akajibu "Alkitaaba wa Sunnah". Maswahaba sisi tutawafuata kwa yale waliyoafikiana na Quran na hadithi za Mtume Swalla Llaahu alayhi wa sallam.*Awi-L-Ijmaanh aw inkaana aswaaha fil Qiyaas],* au ikiwa imesihi kwenye Qiyaas.

Lakini ikiwa haikusihi kwenye Qiyaas wao maswahaba hawawafuati. Hiyo ni kauli ya imamu Shaafiy. Hapa sasa inadhihirisha kuwa Ibnu Abbas haendi kwa swarakha ya aya na hadithi; kwamba mwezi ukionekana sehemu moja sehemu nyengine wasifuate.

Kwa hivyo *Qauli swahabiy* hapa inaweza kurejeshwa. Si kurejeshwa tu kwa vile sisi si masheikh na kwamba tunawarejesha maswahaba, ni kwa sababu hata imamu Shaafiy mwenyewe amesema hivyo.

Hayo yamesemwa vile vile kwenye vitabu vyengine vya fiqhi. Kwa marejeo zaidi mtu anaweza kuangalia kwenye **Al-Waadhih fiy usulil fiqh** cha Dkt Al-Ashqaar na Usulul fiqh cha Abu Zuhra. Watu watakuta huko kuwa Qauli swahabiy zinaweza kurejeshwa ikiwa zipo swahihi za aya na hadithi.

Kuzikataa kauli za maswahaba kukiwa na ushahidi, ni mambo yalikuwepo tangu wakati wa maswahaba. Na sasa wanachuoni mbalimbali wamezungumza hilo. Kufanya hivyo si kwenda kinyume na mafunzo ya Uislamu.

La mwisho kabisa**……..** *kabla kuendelea akamgeukia mwenyekiti na kumuuliza.* Bado dakika ngapi sheikh?. Mwenyekiti akamjibu Endelea, Bismillah. Naye akaugeukia ukumbi na kusema;

Nilikuwa nataka nizungumze habari ya kuonekana mwezi katika dunia na kwamba suala hili si katika ikhtilafu ya kututenganisha sisi.

Akainuka kutoka kitini alipokaa na kuelekea ubaoni. Mwenyekiti akamuhimiza afanye upesi muda wake, umekwisha.

Mtoa mada akamuashiria mwenzake na kuletewa karatasi kubwa jeupe lililokuwa na mchoro uliotayarishwa kabla. Kwa kutumia gundi la waraka akalibandika ubaoni. Kwa kutumia fimbo nyembamba akaanza kuuelezea mchoro wake.

Mchoro wenyewe ulikuwa umepewa jina la SURA ZA MWEZI.

Katikati pamechorwa duara kubwa lililopewa jina la DUNIA. Limegawanywa na mstari uliokaa kwa marefu na kutoa nusu mbili. Nusu ya kulia imepewa jina la mchana na ile ya kushoto ikaitwa usiku.

Kulia ya duara lote la dunia kuna miale inayopiga kutoka eneo lililopewa jina la JUA. Kuzunguka dunia ni michoro ya duara ndogo ndogo na nusu duara, jumla zipo saba na ndizo sura za mwezi.

Sura ya 7 ni kama upinde, uko chini ya miale ya jua kuliani mwa dunia. Maelezo ya mtoa mada yalianza kwa kuifafanua sura ya 7 ya mwezi katika mchoro wake. Hiyo alisema ni pale mwezi unapokuwa umekamilisha safari ya kuizunguka dunia kwenye njia yake (orbit).

Baada ya hapo unaingia katikati ya miale ya jua.Kwa watu walioko kwenye dunia hawawezi kuuona mwezi, na ndipo inaposemwa mwezi umeingia gizani.

Akaendelea kueleza kuwa, unapotoka mwezi eneo hilo huwa umeandama kwa dunia nzima. Sura ya 1 ya mwandamo, ilioneshwa kwa upinde uliogeuka na kuelekea juu tofauti na ile sura ya 7 iliyoelekea chini. Sura ya mwandamo iko juu ya miale ya jua, kulia ya dunia.

Akasema unapoandama wanaouona mwezi ni wale ambao kwao usiku umeanza.Sio kwamba unaonekana kwa watu wa ulimwengu mzima. Hilo linakubalika.

Tunajua kwamba sheria ya kufunga ina masuala mawili kama ilivyokwishakuzungumzwa na mhadhiri wa mwanzo. Kwanza ni kuonekana kwa mwezi na pili ni kwa kupelekewa habari.

Madam mwezi ushaonekana na baadhi ya watu sehemu moja ya dunia,inakuwa tayari mwezi umeshaandama.Ikiwa watu walioko upande wa mchana wanasubiri mpaka dunia izunguke na wao ndipo wauone mwezi. Huko inakuwa siyo kuuona mwezi kwa mara ya mwanzo na wala siyo kuandama kwa mwezi tena. Hiyo inakuwa ni kuuona mwezi katika safari zake za kawaida kuizunguka dunia.

Mwezi kitaalamu unaandama mara 1 tu, na daima huwa unaonekana katika maeneo maalum tu. Ama suala kuwa sisi Unguja tukiuona mwezi jee na watu wa Saudia na wao watauona?. Hilo suala halipo na wala halitatokea. Kwa sababu mwezi umo kwenye safari maalum na vituo maalum. Ndipo Mwenyezi Mungu aliposema katka Qur'an Surat Ar-rahman (55) aya ya 5.*{ JUA NA MWEZI HUENDA KWA HISABU*}.
Kwamba kila kitu kina hesabu zake. Na mwezi nao una vituo vyake na sehemu maalum unaoweza kuonekana.
Mtoa mada akaonesha sura na 1 ya mwezi, halafu akasema.
Kutokana na *POSITION* hii ya mwezi ni sehemu za kuanzia Saudia tu na maeneo mengine ya jirani ndiyo yenye uwezo wa kuuona mwezi. Hata wataalamu wamethibitisha hilo.

Haina maana kuwa mwezi lazima uonekane Saudia ndipo watu waanze kufunga na kufungua. Kama ilivyotokea mwezi uliopita, mwezi ulipoonekana kwa mara ya mwanzo Sudan. Wengine wakafungua wote bila kufuata Saudia. Lakini bado kitaalamu mwezi unapoonekana sehemu moja, basi sehemu nyengine inafaa kufuata.

Ni kweli kuwa, mwezi ukionekana kwa mara ya mwanzo sehemu nyengine hawawezi kuuona. Lakini hiyo si hitilafu ya kufanya watu wasifunge au kufungua kwa kufuata mwezi mmoja.

Huku akiendelea na mazungumzo yake akamuashiria tena mwenzake, akateta maumbo kalibu mawili. Moja duara kubwa ambalo ni wastani wa mara 2 ya mpira wa miguu, lililokuwa na rangi ya shaba na kusimamishwa kwenye kisimamia maalum. Umbo la pili lenye rangi nyeusi lilikuwa na ukubwa kama wa mpira wa miguu. Lile kubwa alisema ni dunia na dogo rangi nyeusi ni mwezi.

Kwa kutumia maumbo hayo akatoa maelezo yanayofanana na yale ya kwenye mchoro uliobandikwa kwenye ubao. Ukuta uliokuwa kuliani kwake akajaalia ndiko ulikotoka mwangaza wa jua.

Huku akiwa ameushikilia mwezi kwa mkono wa kulia na mkono wa kushoto umeigusa duania akasema:-
Mwezi unaizunguka dunia. Dunia inajizungusha kwenye axis (mhimili) na yenyewe inalizunguka jua.
Mwezi unapokuwa hapa (kati ya dunia na jua) hauwezi kuonekana. Lakini ukianza kutokeza hapa mwezi (juu kidogo ya dunia na mwangaza wa jua) watu wanaokuwa sehemu hii (mkono wa kushoto ukiashiria sehemu juu ya dunia) ya dunia wanaanza kuuona, na baadae unaendelea na safari yake huku dunia inajizungusha.

Kwa hiyo watu walioko hapa watauona na wale walioko huku hawauoni. Mwezi ukisogea siku ya pili na dunia nayo ishazunguka. Kwa hivyo watu waliokuwa hawakuuona mara ya mwanzo ulipoandama, sasa watauona.

Lakini sasa mwezi huwa umeshaondoka kwenye kituo chake cha kuonekana kwa mara ya mwanzo na kwenda kwenye kituo cha pili.Huko si kuandama kwa mwezi tena bali kuonekana mwezi katika safari zake za kawaida. Kuandama mwezi ni kule kujitokeza kwa mwezi kwa mara ya mwanzo katika kituo chake cha kwanza.

Ndio maana Mwenyezi Mungu kajaalia mwezi katika dunia uwe ni mmoja tu, tofauti na sayari nyengine. Hiyo yote ni kuonesha kuwa mwezi unaandama mara moja na inatosheleza kwa waislamu, waumini wote walioko katika ardhi kufuata.

SHEIKH AMEIR

Baada ya kuondoka Skh Muhsin; mwanafunzi wa Skh Nassor Bacho, akafuatia mzungumzaji mwenye hoja za kibakwata.Akajitamulisa jina lake kuwa ni Ameir.
Kule kwetu, skh Ameir tunamjua kwa jina lake maarufu, kama ni skh Ameir Tajo mdogo. Akamuelekea marehemu skh Ameir Tajo aliyekuwa kadhi mkuu na mufti wa Zanzibar na kuwaambia wanasemina:
Nimezaliwa kwa mzee huyu hapa. Nimesomea kwenye Ma'ahad Saud kuanzia mwaka 1957-1961. *akaendelea.*

Kwa ufupi tutaleta zile nukta zilizokwisha kutolewa ili tusirefushe muda, na wakati wetu ni mdogo kabisa.
Hapa pameletwa aya {*UTAKAYEMFIKIA MWEZI (HUU WA RAMADHANI) NAYE YUKO MJINI BASI AFUNGE }*Albaqara:185.
Sheikh wa kwanza aliichambua sana aya hii. Zikatolewa maana za *hudhuur* na maana zake nyengine zote.Nitamfuata kama alivyotaka yeye, kuwa *shahar* si *hilaal;* ni zile *ayyaam* kuanzia 1,2,3……., Hilo tunakubaliana.

Na *dhwamir* iliyomalizikia na *falyaswumhu* irejee kwenye siku hizo, ingawaje ni *dhwamir* ya mmoja. Kwa sababu hapo ndipo penye nukta tunapopata *jumlat.*
Mtume Swalla Llaahu alayhi wa sallam aliuelezea mwezi kwa njia 2 tu kutokana na aya hii. Kauelezea mwezi mpungufu, kama alivyosema kwenye hadithi ya mwisho iliyosema *Al-shahar tis'u wa ishiiruuna*.Kama sikusahau, Mtume Swalla Llaahu alayhi wa sallam alitumia ishara, *As-shaharu ha kadhaa*.
Sheikh Ameir akaambatisha vidole vya mikono yote miwili, akainua juu na kurudia mara 2. mara ya 3 akainua kama hivyo lakini akapindisha chini dole gumba la mkono mmoja. Alipopindisha dole gumba, akasema huo ni mwezi mpungufu wenye siku 29. Huo ni mwezi wa upungufu kwa njia moja.Mwezi mkamilifu ni kuwa na siku 30.Hatuna njia ya tatu wala njia ya nne. Kwa maana kuwa hatuha siku 28 wala 31. Tuna mpungufu 29 na mkamilifu 30 tu.

Kwa mahala hapo, kama tulivyoishiria hadithi za riwaya za masahaba mbalimbali.

Swahaba Abu Hurayra alitumia tamko la *fa in ghattia* lenye maana ile ile ya *fain ghumiya*. Swahaba Ibnu Abbas alitumia tamko la *fain haa la bainahu wa bainakum*.Ibnu Masoud na wenziwe walitumia tamko la *fain ghumiya*. Zote zina maana moja.
Lakini kuna ziada ndiyo iliyoweka wazi ya …….. *Fa akmi luu L-iddata thalathiin.* Hizi ni njia mbili;29 na 30.

Ikiwa mwenyewe Shaukaniy kama tunavyosema, kasema inayumkinika kuandama 29 mara 4. Kama sisi tunavyoona *fi-in-laan*] kinadharia. 29 mara 3 tumeona tangu kuzaliwa. Na mara 4 pia tunakubali. Lakini jamani 29 mara zote 12!. Ndivyo hivyo?.
Kweli Mwenyezi Mungu anatwambia katika Qur'an, Surat Tawba aya ya 36.
{HAKIKA IDADI YA MIEZI KWA MWENYEZI MUNGU NI MIEZI KUMI NA MBILI KATIKA HUKUMU YA MWENYEZI MUNGU TANGU ALIPOUMBA MBINGU NA ARDHI, KATIKA HIYO IKO MINNE MITAKATIFU. HIYO NDIYO DINI ILIYO SAWA. BASI MSIDHULUMU NAFSI ZENU HUMO. NA PIGANENI NA WASHIRIKINA WOTE KAMA WANAVYOPIGANA NANYI NYOTE, NA JUWENI KUWA MWENYEZI MUNGU YU PAMOJA NA WACHAMUNGU}.
Miezi kweli ni 12, na jinsi inavyoandama ni kama ilivyo kwenye aya aliyoileta ndugu yetu hapa.Aya ya 189 Suratul Baqara *{WANAKUULIZA KHABARI YA MIEZI. SEMA: HIYO NI VIPIMO VYA NYAKATI KWA AJILI YA WATU NA HIJA …….}.*

Kuwa miezi hiyo 12 haikuwekwa *puruu* tu. Iwe siku 366 hazina tafsiri. Ndipo imeletwa miezi kuandama, ili ipatikane tafsiri. Nini hikma ya aya hapo juu. Ni kuwa watu waweze kujua nyakati za ibada zao, kama alivyo kwisha kutueleza sheikh.

Na nyakati za ibada haziwezi kupatikana kwa watu wote kwa wakati mmoja. Ijapokuwa sheikh hapo alitumia hadith iliyosema *swuumuuu.*Hapo dhwamir ya waw ya *jam'u* kwamba wanaelekezwa waislamu wote.Na kwa hivyo basi waislamu wa dunia nzima. Laa!,Sio kwa maana hiyo.Kwa sababu *dhwamir* za aina hiyo zimo kwenye aya kadhaa.Na kila mmoja itamuhusu kwa wakati wake.

Mfano tunaambiwa *Fa aqimuu swalaa*… Qur'an 22;78. Pia *wa aqimuu swalaa* Qur'an 24:56.Si *dhwamir* ya mmoja;ni ya wengi. Lakini kila mmoja atasimamisha swala kwa wakati wake.Ndipo aya ya 78 surat bani Israil ikasema:
{SHIKA SALA JUA LINAPOPINDUKA MPAKA GIZA LA USIKU.NA QUR'AN YA ALFAJIRI INASHUHUDIWA DAIMA}. Yaani kila mmoja atafuata wakati wake huo.

Ata-aniy mina Rahmaan. Nilifurahi sana sheikh pale alipoleta *ata-aniy*, pamoja na kwamba *al-ajalat mina shaittaan*. Lakini kukubali nikaja tena mimi.

Nukta aliyoichengea imenisaidia sana mimi. Kama alivyoeleza kijana. *Akatumia mkono wake mmoja na mikrofoni kama mfano akasema* " Ikiwa mwezi ni huu na jua ni hili. Na ukizunguka huku hauonekani. Ndipo hapa tunapopapigania".
.

Wewe ukipitwa na dakika 20 tu, au dakika 30; nusu saa. Ukija kudhihiri na kuuona. Wewe huuoni nchi ile kwa sababu umeshaingia tena haupo.

Mwezi tisa wa ishirini ni mdogo kabisa. Ndipo aliposema sahaba *Fa akmiluu L-iddata thalathiin*] Kamilisheni hesabu, mwezi 30, siku thalathiini.Huna tena nja ya kusema kuwa tumeuona kwa dunia nzima.

Masahaba Abu Hurayra, mstari wa mbele, Ibnu Abbas wa mstari wa mbele na Sayyid Abdullah ibnu Masoud wa mstari wa mbele.

Wako wajuzi zaidi kuliko ndugu zetu hawa waliokuwa mstari wa mbele katika kumjua Mtume Swalla Llaahu alayhi wa sallam na kuzijua aya?. Iwe sisi ndio tunaijua aya zaidi!.

Kwa kurejea. Ipo *mafhuum*. Naondoa tuhuma katika ile hadithi ya Kuraib. Mara nyingi huwa tunasikia vichochoroni. Hapa leo hawakuileta tafsiri ile. Na tulitaka iletwe.

Katika hadithi ya Kuraib yapo maneno aliyoyasema *Alaa taktafiy bi ru'yat Muawiya wa swiyaamih?].* Hujitoshelezi kwa kuuona balozi, swahaba mkuu Muawiya? huko Shaam na kufunga kwake?.

Pale Abdulla ibnu Abbas alijibu Laa!]. Hii Laa hapa kaondoa sentensi (jumla) nyingi. Sio maana ya mbele. Sio *Laa hakadhaa amaranaa RusuuuluLlaah.*Laa! *Bi maana Laa naktafiy bi ru'yat Muawiya wa swiyaamih*. *Hakadhaa amaranaa RasuuluLlaah, swuumuu Li ru'yatih wa afttiruu Liru'yatih.*

Sio Laa hakadhaa amaranaa RasuuluLlaah.Laa!. Pana maneno.
Mfano nikikwambia, utachukua boksi la chaki?. Wewe ukaniambia. Laa!. Basi Laa hii inajibu maneno, maana yake sichukui.

Kwa hivyo aliposema *Alaa taktafiy bi ru'yat Muawiya wa swiyaamih?.* Yeye akajibu Laa. Maana yake *Laa aktafiy bi ru'yat Muawiya wa swiyaamih]*. Siyo *Laa hakadhaa amaranaa Rasuuilillah.* Ile ni jumla nyengine.

Ndugu!, Ilikuwa tusirefushe, lakini pahala pa nukta. Kusema jee ikiwa siku zote sisi iwe umeandama faur, umeandama popote, pote ni 29, miezi 12 utaandama 29 tu, hakuna 30?. Na Mtume Swalla Llaahu alayhi wa sallam kaashiria na 30 pia. Wazee!, Itakuwa wapi tutaipeleka miezi 12?.

Skh Ameir alipofika hapo, akaja mjumbe kutoka meza kuu akanong'ona naye….-. Mwenyewe mtoa mada akiwa ametabasamu na kuonekana na hamu ya kuendelea na mchango wake akasema :-

Naam!, kwa hivyo naondoa shubha nyengine. Amri ya *swuumuu*. *Dhwamir* hii, na wale walioleta mambo ya *Usuuli* na *Qiyaas*.Kama alivyothibitisha yeye mwenyewe kuwa hiyo Qiyaas na *ijmaa- anh* ni katika Qur'an. Lakini *Qiyaas* ziko nyingi. Kuna *Qiyaas Aulawiy*, *Qiyaas mustawaa*. *Qiyaas adnaa*.

Na ikawa imeletwa *Qiyaas Adnaa*; ya chini, kuipeleka juu na wepesi. Tuna weza kuifahamu haraka kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika surat Bani Israail (17) aya ya 23. *{NA MOLA WAKO AMEHUKUMU KUWA MSIMUABUDU YOYOTE ILA YEYE TU. NA (AMEUSIA) KUWAFANYIA WEMA WAZAZI WAWILI (BABA NA MAMA) KAMA MMOJA WAO AKIFIKIA UZEE (NAYE YUKO) PAMOJA NAWE, AU WOTE WAWILI, BASI USIWAAMBIE HATA AH! WALA USIWAKEMEE NA USEME NAO MANENO MAZURI (YA HESHIMA)}*

Tumekatazwa kuwaambia wazee wawili hata kuwaambia upuuzi; kedda !.

Sasa hapo kwenda juu utafahamu. Pumzi gani iko juu; ni kubwa zaidi kuliko kuwaambia upuuzi. Kuliko tungekatazwa la juu kwenda chini. Ukikatazwa dogo na kubwa linaingia wenyewe.

Kwa hivyo *Qiyaas* inaingia katika Qur'an na *Qiyaas* ni Qur'an kamili na *ijma – anh*., wote wafahamu.

Mattali'i siyo kweli kuwa hayakutajwa katika Qur'an.Na mwenyewe umethibitisha hapa. *Mattaali'i* ya jua tu. Sayari kubwa ni jua. Sasa huo usiku na mchana tunaupata kwa kitu gani?; si ni kwa jua!. Ilivyokuwa haupatikani mwezi mpaka lije jua lifanye kazi, kwa hivyo na mwezi nao una *mattaali'i.*

Kufika hapo meza kuu ikagongwa kutoa ishara kuwa muda wake umekwisha. Mwenyewe, mtoa mada akainua mikono kuashiria kuwa amefahamu na anandoka.

Huo ukawa ndio mwisho wa mjadala wa mwezi uliochukua muda mwingi katika semina hiyo.

Kabla kuingia mjadala wa kufaa au kutokufaa kwa Maulidi, mwenyekiti wa semina akatoa historia fupi ya ushirikiano na mafahamiano ya waislamu Zanzibar. Akawataja masheikh mbali mbali ambao pamoja na ikhtilafu na kuwa na rai tofauti baina yao bado walikuwa wakitembeleana misikitini mwao.

Mwenyekiti, Skh Ahmed Zubeir akaufunga mjadala wa mwezi kwa beti fupi ambazo alisema alizipata kutoka kitabu fulani cha histrora alichokisoma zamani huko huko Zanzibar.

ALLAHU AKBAR, JAISHUL ILMI YANHAZIMU BI ZINJIBARI, WA JAISHU JAHLI JARRAAU.

Nimezifahamu beti hizo kwa maaana ya

MWENYEZI MUNGU NI MKUBWA. JESHI LA WENYE ELIMU LIMESHINDA ZANZIBAR, NA JESHI LA WAJINGA LIMESAMBARATIKA.

……

Baada ya kuusoma mjadala wa mwezi wa Eacrotarnal tuma kura yako juu ya nani walishinda baina ya Ansaar Sunnah na Bakwata.Tumia anuani yoyote kati ya zilizoorodheshwa katika Contact us**:*www.islamicalendartides.com*.**Matokeo yatakuwa yakichapishwa kila baada ya muda inshaAllah.